# Nipashe

Jumatatu Julai 13, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580282

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO

'Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka'

USICHUKULIE POA UNATEGEMEWA


## ACT-Wazalendo yatamba kushinda uchaguzi Z'bar



UKURASA 3

# Sababu JPM kupata kura 100% zatajwa

• **Wana-CCM** Zanzibar wafunguka uteuzi wa Dk. Mwinyi...*Endelea ukurasa 2,4*



Baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi CCM pamoja viongozi wengine wakiweka zege kama kumbukumbu katika ujenzi wa ofisi mpya za Ikulu ya Chamwino, Dodoma, jana. **PICHA: IKULU**

## Mambo 6 muhimu Ilani CCM 2020-2025

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Mkuu wa Anglikana atema cheche kuelekea uchaguzi

UKURASA 2

**MICHEZO** TANZANIA CHALI, UGANDA YAPETA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Askofu atema cheche kuelekea uchaguzi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MKUU wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Askofu Maico Mndolwa, amekemea baadhi ya waumini kuingiza suala la siasa kanisani na kuwaonya wenye tabia ya kuingia na nguo za vyama kwenye nyumba za ibada kuacha mlangoni ili kulinda amani na kuepuka machafuko.

Askofu Mndolwa alitoa kauli hiyo jijini hapa jana, katika ibada maalumu ya kuliombea taifa iliyofanyika Kanisa Kuu la Mtakatifu Nicholas, Dayosisi ya Victoria Nyanza (D.V.N).

"Wanasiasa mnapoingia makanisani ingieni kama waumini kwa unyenyekevu mkubwa, sio kufanya nyumba za ibada majukwaa ya siasa, kazi za nje zitumike nje na sio sehemu takatifu tusidhalilishane, tusioneane na tusileteane kejeli za viwanjani na vijiweni kanisani kwa sababu ya siasa," alionya Mndolwa.

Askofu Mndolwa alisisitiza kuwa, kanisani wanasali kwa kumuahidi Mungu na sio suala la siasa na kuwataka waumini wenye wagombea wao wamalizane nje badala ya kuingiza kwenye nyumba za ibada.

"Tunawaomba sana wagombea wanapokuwa majukwaani kuomba kura, waache lugha za matusi, kejeli na vijembe na watambue tuna watoto katika taifa hili wanaotaka kusikia mambo mema na sio maovu, tunahitaji kujenga vijana walio na maadili kwa kutumia lugha zenye staha," alisema.

Vile vile, Mndolwa alisema mwananchi asipotimiza wajibu wa kuchagua viongozi bora, atakuwa amejinyima haki yake na kushindwa kumtukuza Mungu na kupoteza amani, haki hutimizwa na wajibu na ndipo hupatikana amani na ikiminywa inatoweka, tabu na shida zinajitokeza.

"Tunamshukuru Mungu katuvusha katika magumu na nchi yetu inapiga hatua katika mambo ya kiuchumi, kisiasa na amani safi na kupambana na janga Covid-19, Mungu atupe viongozi wenye maono na uchungu wa nchi yetu walio na utayari wa kusaidia watu," alisema Mndolwa.

Aliwataka wagombea wanawake kuacha kutumia miili yao kwa ajili ya kupata uongozi na kuwakumbusha watambue kufanya hivyo wanakuwa sio viongozi walioteuliwa na Mungu, katika kipindi chao cha madaraka misukosuko itakuwa mingi kwa kuwa hawakutunukiwa na Mungu kuongoza jamii.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akisaidiana na wafugaji kuswaga ng'ombe ili waweze kuingia kwenye kibanio cha kuchanjia kupatiwa chanjo ya kinga ya ugonjwa wa homa ya mapafu. **HABARI UK. 4. PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Sababu za JPM kupata asilimia 100 zaanikwa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WACHAMBUZI wa masuala ya siasa nchini wamesema kitendo cha Rais John Magufuli kutekeleza ahadi nyingi alizozitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2015, ndiyo sababu iliyowashawishi wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kumpigia kura za asilimia 100.

Wamesema miaka mitano ya uongozi wake, Rais Magufuli amefanya siasa za sayansi, hali iliyowashawishi wajumbe kuwa na imani na kutaka aendelee na awamu ya pili ya miaka mitano.

Juzi, wajumbe wote 1,822 wa chama hicho wakiwa mjini Dodoma katika mkutano mkuu, walimpigia kura za ndiyo Rais Magufuli kuwania tena nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu wa Oktoba kwa tiketi ya CCM.

Wakizungumza na Nipashe, wachambuzi wa masuala ya siasa nchini wameeleza kuwa ushindi alioupata Rais Magufuli ndani ya chama chake umedhihirisha namna anavyokubalika kutokana na utendaji kazi wake.

Dk. Richard Mbunda, kutoka Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema halikuwa jambo geni kwa Rais Magufuli kupitishwa kwa kishindo na mkutano mkuu na kwamba ilikuwa inatarajiwa kutokea.

Alisema: "Chama kilikuwa na imani kubwa naye kutokana na siasa zake alizofanya akiwa madarakani, kuna siasa na siasa, pia kuna siasa za kisayansi. Sasa Rais Magufuli alifanya siasa za kisayansi ambazo utekeleza kile ulichoahidi, Yeye (Rais Magufuli) ametekeleza ahadi nyingi alizozitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Hivyo wajumbe wasingeshindwa kumpitisha kwa kishindo."

Aliongeza kuwa mwaka 2015 CCM ilipoteza mvuto pamoja na mwelekeo, lakini baada ya Rais Magufuli kuingia madarakani imerudisha mvuto, vijana wengi wamejiunga na chama hicho, na hata baadhi walioku-wa upinzani wamerejea.

"Wanachama wa CCM walikuwa hawavai sare mtaani wanaogopa, wakivaa walikuwa wanazomewa, lakini sasa hivi wanashona hadi nguo. Rais Magufuli amekirudisha kwenye ramani," alisema Dk. Mbunda. Kuhusu Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), pamoja na Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, kumpitisha Dk. Hussein Mwinyi kuwania urais visiwani Zanzibar, Dk. Mbunda alisema: "Tulitarajia angepata uteuzi huo, ni mtu ambaye anaungan-isha Bara na Zanzibar."

Dk. Mbunda alisema Dk. Mwinyi ni mtu asiyejikweza tofauti na wagombea wengine na pia anafanya kazi bila ya kelele.

Mchambuzi wa masuala siasa na Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Kanisa Katoliki cha Ruaha (RUCU), Prof. Gaudence Mpangala, alisema wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM walikuwa wanamkubali Rais Magufuli kwa utendaji wake.

Prof. Mpangala alisema Rais Magufuli tangu alipokuwa Mwenyekiti wa CCM, ameweza kuleta mabadiliko ndani ya chama hicho pamoja na Taifa.

"Rais Magufuli ameweza kubadilisha muundo wa chama, amepunga idadi ya wajumbe, ameweza kupambana na rushwa ndani ya chama na serikalini, hivyo ilikuwa ni lazima apitishwe kwa kishindo."

Kuhusu Dk. Mwinyi, Prof. Mpangala alisema: "Nilitarajia angechaguliwa tu. Kati ya wagombea 31 waliojitokeza kuchukua fomu utendaji kazi wao walikuwa hawamfikii Dk. Mwinyi."

Alisema Dk. Mwinyi amekuwa ni kiongozi katika ngazi ya muungano, amedumu vizuri katika wizara alizoziongoza pia ni mwanasiasa aliyetulia na hana haraka.

Naye mchambuzi wa masuala ya siasa, Deus Kibamba, alisema hakushangazwa na hatua ya wajumbe wa mkutano mkuu kumpitisha kwa asilimia 100 Rais Magufuli.

Kibamba ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), alisema Rais Magufuli anakubalika kwa asilimia kubwa ndani ya CCM, na kwamba hilo halina ubishi.

Alisema hata angetokea mgombea wa kushindana naye ndani ya chama, Rais Magufuli angeshinda kwa asilimia zaidi ya 60.

Kuhusu Dk. Mwinyi kuchaguliwa, Kibamba alisema: "Atakuwa kiongozi wa kawaida na siyo machachari. Kwa Zanzibar namna ilivyo ataimudu, Ni mchapakazi. Wazanzibar wategemee kumpata Rais ambaye yuko kama Rais Dk. Ali Mohamed Shein."

Naye Mhadhiri wa Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma wa UDSM, Dk. Muhidin Shangwe, alisema ilitegemewa Rais Magufuli kupita kwa kushindo kwa sababu alikuwa ndiye mgombea pekee.

Alisema wajumbe wa mkutano mkuu walikuwa na imani naye kiongozi huyo, na kwamba isingekuwa rahisi kutompitisha.

Kuhusu uteuzi wa Dk. Mwinyi, Dk. Shangwe alisema: "Aliandaliwa 'kusave' (kuhudumu) Zanzibar kwa sababu aliongoza wizara nyeti. Ni kama Jakaya Kikwete alivyoongoza Wizara ya Mambo ye Nje kwa miaka 10 na baadaye akawa Rais."

HABARI KITAIFA

# CCM yataja mambo sita muhimu Ilani 2020-2025

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeweka vipaumbele sita katika ilani yake kwa mwaka 2020-2025, kikiwamo cha kutengeneza ajira zisizopungua milioni nane katika sekta rasmi na zisizo rasmi, hususani kwa vijana.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiru Ally, alieleza hayo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa kupitisha jina la mgombea urais, uliofanyika jijini Dodoma na kuhudhuriwa na wajumbe 1,822 wa chama hicho.

Dk. Bashiru alisema kwa mujibu wa Katiba ya CCM, Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), ndiyo chombo kinachoandaa na kupitisha mwelekeo wa sera za chama pamoja na ilani.

Alisema Kamati Kuu ya CCM ilifanya kazi yake na kuwasilisha nyaraka hizo mbili na NEC ilipitisha ilani ya chama hicho kwa mwaka 2020-2025 pamoja na mwelekeo wa CCM kwa mwaka 2020-2030.

Alivitaja vipaumbele vya ilani hiyo kuwa ni kulinda na kuimarisha misingi ya utu, usawa, haki na uongozi bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa taifa na muungano.

Alitaja kipaumbele kingine ni kukuza uchumi wa kisasa jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa viwanda huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi.

Kingine ni kuleta mapinduzi ya kilimo, mifugo na uvuvi, ili kuwapo na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu kwa maendeleo ya taifa.

Dk. Bashiru alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji, umeme na makazi bora mijini na vijijini.

Alisema, kipaumbele cha sita ni kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi na teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya haraka kijamii na kiuchumi.

MAREKEBISHO YA KATIBA

Dk. Bashiru alisema NEC pia imependekeza kufanyika kwa marekebisho madogo katika Katiba ya chama hicho ya mwaka 1977 toleo la Julai, 2017.

Alisema maeneo makubwa mawili ndiyo yaliyofanyiwa marekebisho kutokana na sababu za mabadiliko ya sheria za vyama vya siasa, lakini mapendekezo yaliyotoka katika Kamati Kuu na NEC.

Dk. Bashiru alisema: "Kufuatia kuanza kutumika kwa sheria hii, Msajili wa Vyama vya Siasa ameviitaka vyama vya siasa kuanza kurekebisha katiba za vyama vyao maeneo ambayo ibara za katiba zao zinakinzana na vifungu vya sheria za vyama vya siasa sura ya 258 ya mwaka 2019."

CCM kwenye katiba yake toleo la mwaka 2017 ina ibara kadhaa ambazo alisema zinakidhi matakwa ya sheria ya vyama vya siasa. Hata hivyo zipo ibara chache zinazopaswa kufanyiwa marekebisho.

Dhumuni la marekebisho hayo alisema ni kuendana na mageuzi makubwa ya kasi ya kisiasa na utendaji ndani ya chama kuna mapendekezo mengine ambayo yanapaswa kuingia katika katiba.

Pia, alisema Halmashauri Kuu ilipendekeza marekebisho katika maeneo makubwa mawili, mojawapo ni kuwajumuisha wenyeviti wa mashina (mabalozi), kushiriki katika mikutano mikuu ya kata na wadi ili kupiga kura kwa wagombea wa udiwani.

Alisema lengo ni kuwawezesha viongozi hao waweze kushiriki katika kura za maoni kwa viongozi ngazi ya vitongoji, mitaa, vijiji na kata na wadi kwa upande wa Zanzibar.

# ACT yatamba kushinda uchaguzi wa Zanzibar

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema kimejipanga vyema kuibuka na ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, hasa nafasi ya urais visiwani Zanzibar.

Vilevile, kimesema hakibabaishwi na mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) aliyepitishwa na Halmashauri Kuu ya chama hicho, jijini Dodoma Ijumaa iliyopita, Dk. Hussein Mwinyi.

Akizungumza na The Guardian Digital muda mfupi baada ya kupitishwa kwa mgombea wa CCM, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, ametamba kuwa mgombea waliyemwandaa hawezi kushindwa uchaguzi huo kwa kile alichodai kuwa ana uzoefu wa kutosha katika siasa za Zanzibar.

"Dk. Mwinyi ni mtu ambaye tunafahamu uwezo wake na udhaifu wake na kwetu sisi ni mgombea ambaye ni dhaifu zaidi kwa hiyo hatubabaishi na tutapata ushindi mnono," alibainisha Shaibu.

Tayari Mwenyekiti wa chama hicho Maalim Seif ametangaza atawania urais katika chama hicho, ikiwa ni mara ya sita kuwania urais katika visiwa hivyo kupitia Chama cha Wananchi (CUF) mara tano na kupitia ACT-Wazalendo kwa mara ya kwanza.

Ijumaa iliyopita CCM ilimpitisha Dk. Mwinyi kuwa mgombea urais wa chama hicho katika visiwa vya Zanzibar baada ya kupata asilimia 78 ya kura zote za wajumbe hao na kuwashinda wagombea wengine wawili.

Dk. Mwinyi ni mtoto wa Rais mstaafu wa awamu ya pili wa Tanzania, Alhaji Ali Hassan Mwinyi na alishika nyadhifa mbalimbali katika serikali kuanzia awamu ya tatu iliyoongozwa na Rais mstaafu Benjamin Mkapa hadi sasa inayoongozwa na Rais John Magufuli.

Nafasi yake ya mwisho kushikilia ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.



# Wazanzibari wafagilia uteuzi wa Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADHI ya wananchi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar wamesema mgombea urais kupitia chama hicho, Dk. Hussein Mwinyi ni chaguo sahihi kwa sababu ana uzoefu mkubwa wa uongozi katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza na Nipashe, Iddi Haji mwanachama wa CCM, alisema mgombea huyo aliyepitishwa mwishoni mwa wiki ana uwezo na sifa za kupambana na upinzani katika uchaguzi mkuu wa urais wa Zanzibar unaotarajiwa kufanyika Oktoba.

"Dk. Mwinyi ni msomi, aliyepikika na kuyajua Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964 na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kama ndiyo tunu za kitaifa," alisema Haji.

Haji Suleiman, mkazi wa Michenzani Mjini Unguja, alisema Zanzibar inahitaji kiongozi atakayefanya kazi kubwa ya kuwaunganisha watu mbalimbali bila kujali itikadi zao za kisiasa na ukabila.

"Wananchi wa Zanzibar wanahitaji Rais ambaye atafanya kazi kubwa ya kuwaunganisha watu mbalimbali bila ya kujali itikadi za vyama vyao...wakati wa harakati za uchaguzi Wazanzibari hugawanyika kwa imani za vyama vya siasa na kusahau maendeleo," alisema.

Muhamed Jongo, mfanyabiashara katika eneo la Darajani Unguja, alimtaka mgombea huyo endapo atapata ridhaa ya wananchi kuiongoza Zanzibar kuendelea na mikakati ya kuimarisha sekta ya biashara na kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara huria.

Alisema sekta ya biashara bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo tatizo la kodi na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara.

"Wazanzibari kwa asilimia kubwa ni wafanyabiashara, tunataka kuona yanakuwapo mazingira mazuri yatakayotuwezesha kufanya biashara vizuri bila usumbufu wa kodi," alisema. Fatuma Juma, mkazi wa Kombeni Zanzibar, alisema Dk. Hussein anaweza kupambana na upinzani na kuiletea ushindi wa kishindo CCM katika uchaguzi wa Oktoba.

"Sina wasiwasi na mgombea aliyechaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM (NEC)...najua anao uwezo na sifa pamoja na vigezo vitakavyomwezesha kukivusha Chama Cha Mapinduzi na kushika dola," alisema.

**ACT: HATUNA TATIZO NAYE**

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano ya Umma ya Chama cha ACT-Wazalendo, Salim Bimani, alisema wameupokea uteuzi wa Dk. Hussein Mwinyi ambaye watakutana naye katika majukwaa ya kisiasa katika kipindi cha harakati za kampeni za uchaguzi mkuu.

"Sisi hatuna matatizo wala shaka na mgombea wa CCM Dk. Hussein Mwinyi...tunamkaribisha katika harakati za kisiasa na kampeni za uchaguzi mkuu ambapo tunaomba tufanye kampeni za kistaarabu zitakazowaunganisha wananchi na sio kuwagawa," alisema.

Alisema mgombea huyo hajawa tishio kwa chama cha ACT-Wazalendo kwa sababu chama hicho kina hoja madhubuti.

**ADA TADEA YAMPONGEZA**

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ADA TADEA, Juma Ali Khatib ambaye ni mgombea wa urais kupitia chama hicho, alimpongeza Dk. Hussein Mwinyi kwa kuibuka mshindi katika kinyang'anyiro, huku matarajio yake makubwa kuwapo kwa kampeni na sera zitakazojikita kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na maendeleo.

"Ni chaguo sahihi, ni kiongozi mwenye hekima na busara mwenye uzoefu wa kuongoza katika wizara mbalimbali za Muungano akiwa pia mwakilishi wa wapigakura Jimbo la Kwahani kwa zaidi ya miaka 15...sisi tutampa ushirikiano mkubwa na kufanya kampeni zitakazojenga umoja na mshikamano," alisema.

**AAFP YAPONGEZA UTEUZI**

Mwenyekiti wa Chama cha AAFP Said Soud ambaye ni mgombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho, alisema AAFP kinawapongeza wana CCM kumchagua Dk. Hussein Mwinyi kuwa mgombea wao.

"Mazingira ya kisiasa ya Zanzibar yanafahamika, hivyo nawaomba Wazanzibari kuwa watulivu ili kuendesha shughuli za kisasa na kuchagua viongozi wanaofaa kuiongoza Zanzibar," alisema.

Alisema ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha amani na utulivu uliojengeka katika misingi ya Dk. Ali Mohamed Shein inaendelezwa kwa sababu demokrasia sio ugomvi wala sio mfarakano bali ni haki ya kuchagua au kuchaguliwa.



Askari wa usalama barabarani akishirikiana na raia kupima ajali ya pikipiki na gari iliyotokea mtaa wa Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ponda ashikiliwa tuhuma za uchochezi

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia Katibu Mkuu wa Shura Maimamu Tanzania, Sheikh Ponda Issa Ponda kwa mahojiano.

Sheikh Ponda anahojiwa kwa madai ya kuandika waraka wa kichochezi.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alithibitisha kushikiliwa kwa Ponda, kutokana na waraka uliotolewa hivi karibuni na taasisi hiyo ya Shura.

"Ni kweli tunamshikilia Sheikh Ponda na tunamhoji kwa tuhuma za uchochezi," alisema.

Inadaiwa kwamba viongozi wote wa taasisi hiyo wamekana kuhusika na waraka huo isipokuwa Ponda.

Amiri Mkuu wa Shura ya Maimamu, Sheikh Mussa Kundecha, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, alikana uongozi wa taasisi hiyo kutoa waraka wowote na kuusambaza kwa vyombo vya habari.

"Tulipata taarifa kwamba kuna waraka ambao tumeutoa unaohusu uchaguzi ambao tumeusambaza kwenye vyombo vya habari, mimi kama Amiri Mkuu wa Ashura ninayetambulika kitaifa, nasema hatujatoa waraka na Baraza Kuu halijatoa waraka huo katika kipindi hiki," alisema Kundecha.

# Bei elekezi uchanjaji mifugo yasisitizwa

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

SERIKALI imewataka wadau wote wanaojishughulisha na uzalishaji, usambazaji na uchanjaji wa mifugo kuzingatia bei elekezi zilizotangazwa na serikali na atakayekwenda kinyume atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Luhaga Mpina, kwa niaba ya serikali alitoa onyo hilo wakati wa uzinduzi wa chanjo za kimkakati 13 za mifugo kitaifa.

Waziri Mpina alisema juhudi zinazofanywa na serikali haziwezi kupotea bure na kuonya halmashauri zitakazozembea kusimamia utoaji chanjo hizo.

Alisisitiza kuwa chanjo ya mifugo sio la hiari tena bali ni jukumu la kisheria kupitia kanuni ya chanjo na uchanjaji ya mwaka 2020 chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya mwaka 2003 ambayo inamtaka kila mfugaji kuchanja mifugo yake dhidi ya magonjwa ya kipaumbele kulingana na kalenda ya chanjo iliyotolewa na wizara.

Akizungumza wakati wa uzinduzi kampeni ya chanjo hiyo katika Kijiji cha Kinyangiri, Wilaya ya Mkalama Mkoa wa Singida, Waziri Mpina aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri 82 za wilaya ambao hawajaanza uchanjaji na zile zinazosuasua kuanza mara moja vingine hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao kwa kurudisha nyuma jitihada za serikali katika kuleta mageuzi ya sekta ya mifugo.

Pia Waziri Mpina ameagiza wataalamu wote wa mifugo ngazi ya wizara, mikoa, wilaya na kata kuhakikisha uchanjaji wa mifugo unatekelezwa kikamilifu kulingana na kalenda ya chanjo kwa kuwa jukumu hilo ni la kisheria na kumwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo (DVS), kusimamia kikamilifu na kuwasilisha taarifa ya chanjo kila mwezi kwa waziri na maofisa ambao wameshindwa kusimamia utoaji wa chanjo hatua kali zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili.

Kuhusu madeni ambayo halmashauri zinadaiwa na Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) yanayokadiriwa kuwa Sh. milioni 125, Waziri Mpina ameagiza ifikapo Agosti 30, wawe wamelipa na wakishindwa kufanya hivyo halmashauri hizo zifikishwe mahakamani, huku serikali ikimfuatilia mkurugenzi husika uwezo wake wa kusimamia majukumu ya serikali.

TANGAZO


# Shukrani kwako Mlipakodi!

TRA

## Haya yote yamefanyika kutokana na kodi yako!

Ujenzi wa barabara za juu/Flyovers



Ujenzi wa reli ya Standard Gauge (SGR)



Ujenzi wa barabara ya Chunya-Mbeya



Ukarabati wa meli ya MV. Victoria




Maboresho Sekta ya Afya



Ukiuza toa risiti, ukinunua dai risiti

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni Ligi Kuu msimu ujao ziboreshwe kisasa

**KUMALIZIKA** kwa msimu huu wa mwaka 2019/20, ni ishara sahihi kuwa maandalizi ya msimu mpya wa 2020/21 yanatakiwa kuanza mapema.

Tayari kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imesh-acheza mechi 34 kati ya michezo 38 ambayo inatakiwa kuchezwa kwa kila klabu.

Simba ya jijini, Dar es Salaam tayari imeshatwaa ubingwa wa ligi hiyo wakati vita iliyobaki ni ya timu zinazopambana kujinasua na janga la kushuka daraja.

Ushindani huo umekuwa mkubwa kutokana na mabadiliko ya kanuni yaliyofanywa kabla ya kuanza kwa msimu, kati ya timu 20, nne zitakazoburuza mkia zitashuka moja kwa moja wakati mbili zitacheza mechi za mtoano na klabu nyingine mbili za Ligi Daraja la Kwanza.

Kwa upande wa Ligi Daraja la Kwanza, tayari Gwambina FC kutoka Misungwi ya jijini, Mwanza na Dodoma Jiji FC tayari zimeshapanda daraja, zitacheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Moja ya mambo muhimu yanayotakiwa kuwekwa sawa ni kanuni za Ligi Kuu Bara na kanuni hizo huandaliwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kufuata mapendekezo ya wadau wake, ambao ni klabu.

Timu zote zinatakiwa kutumia muda wa maandalizi ya kanuni vizuri ili msimu mpya utakapoanza, kusiwe na malalamiko yoyote ya kuburuzwa au kuonewa na TFF.

Nipashe inaamini klabu zikitumiwa vizuri nafasi ya kuwasilisha maoni yake, tutashuhudia kutosikia malalamiko ya mara kwa mara wakati safari ya kusaka mfalme mpya wa Tanzania Bara atakavyoanza kusakwa.

Klabu zinatakiwa kutoa mapendekezo kuhusiana na idadi ya nyota wa kigeni watakaoruhusiwa kusajiliwa kwa kuzingatia hali halisi walizonazo na si kukubaliana kwa kuzifaidisha klabu chache.

Tunawakumbusha kanuni ya wachezaji wa kigeni ifanyiwe kazi kwa kuzingatia maslahi ya nchi na vile vile ikiwaangalizi nyota chipukizi ambao wanahitaji nafasi ya kukuzwa pamoja na kuendelezwa.

Kwa sasa kanuni zilizopitishwa na TFF, zinataka timu moja kusajili wachezaji wakigeni wasiozidi 10, je, kipindi hiki ambacho Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inategemea zaidi wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu, inastahili kuwa na wageni zaidi au wapungue?

Klabu pia zinatakiwa ziwe mfano kwa kusajili wachezaji wa kigeni wenye viwango vya juu na kuacha kuzifanya klabu zao kuwa sehemu ya majaribio.

Wachezaji wageni watakaosajiliwa wawe ni wenye kuleta ushindani na watakaowapa changamoto ya kuwania namba wazawa ambao ndio wengi zaidi.

Mbali na ushindani wa kuwania namba, pia usajili wao unalenga kuwapa changamoto wachezaji wazawa ili wajitume na waongeze bidii, hatimaye nao kuwindwa na timu za mataifa mengine au kwa walioko katika madaraja ya chini kutakiwa na timu za ngazi ya juu.

Klabu zisione aibu kuwafanyia majaribio wachezaji wao kama ambavyo tunashuhudia klabu za Ulaya zinavyowafanyia nyota inaotaka kuwapa mikataba mpya na kwa kufanya hivyo, Ligi Kuu Bara itapanda thamani na hapo itakuwa ni mwisho wa kusajili 'wababaishaji'.

Pia kuna suala la mgawanyo wa mapato, hii imeonekana kusumbua baadhi ya klabu za mikoani pale wanapokuja Dar es Salaam na kushuhudia timu mwenyeji akivuna kiasi kikubwa tofauti na wanavyokwenda ugenini. Suluhisho ni kuridhia kurudi kwenye mgawanyo wa zamani ambao mwenyeji anapata asilimia 60 na mgeni ataondoka na asilimia 40.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Dodoma FC isipande Ligi Kuu Bara kisiasa

**HATIMAYE** Dodoma Jiji FC ya jijini Dodoma imepanda daraja na msimu ujao wa 2020/21, itashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Dodoma Jiji iliyokuwa kwenye Kundi A, sasa inaungana na Gwambina FC ya Misungwi jijini Mwanza moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Hii si mara ya kwanza kwa mkoa wa Dodoma kupata timu itakayocheza Ligi Kuu, ingawa ni kwa muda mrefu sasa imekuwa haina timu inayocheza kwenye hatua hiyo ya juu.

Katikati ya miaka ya 70, hadi katikati ya miaka ya '80, kulikuwa na timu mbili zilizopishana vipindi zikicheza Ligi Kuu kutoka mkoa huo, nazo ni Waziri Mkuu na CDA.

Timu hizo zilitoa wachezaji wengi wazuri baadhi yao wakiwa ni Justine Simfukwe, Charles Mngodo, Mkala Maulidi, Daniel Poka, Makwa Selemani, Mtemi Ramadhani na Lila Shomari.

Kati ya hao, Lila na Mtemi waliwahi pia kuichezea Simba baada ya kutoka hapo.

Ni heshima kubwa kwa Jiji la Dodoma, ambako ndiyo Makao Makuu ya Tanzania kuwa na timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara, wakati huo mashabiki wa soka nchini wakisubiri kwa hamu kukamilika kwa uwanja mkubwa wa kisasa.

Siku ya Jumamosi niliwasikia mashabiki wa timu ya Dodoma Jiji wakishangilia kwa nguvu, timu yao kupata Ligi Kuu baada ya kuichapa Iringa United mabao 2-0.

Baadhi ya wachezaji wake ambao ni wazoefu wa Ligi Kuu ni Emmanuel Mseja ambaye alishawahi kuichezea Mbao FC na Simba. Ni baada ya kutoka Simba ndipo alipokwenda Dodoma Jiji.

Wengine ni Mcha Hamisi aliyekuwa Azam FC, Lipuli na Ruvu Shooting na ndiye aliyefunga bao la kwanza kwenye mechi hiyo.

Wakati shamrashamra za Wanadodoma Jiji ziliendelea, baadhi ya mashabiki wa soka bado wanajiuliza maswali.

Ni kwamba Dodoma Jiji FC imepanda Ligi Kuu kuja kuleta ushindani au kwa sababu za kisiasa tu, kwa sababu tayari jiji hilo limeshatangazwa rasmi kuwa makao makuu na shughuli za kiserikali zimeshahamia huko?

Wana haki ya kujiuliza hivyo. Na hata mimi najiuliza hivyo. Isije kuwa timu inapanda tu kwa sababu za serikali ya jiji hilo ilifanya kila njia ili jiji hilo nalo lipate timu ya Ligi Kuu tu basi na badala ya hapo hakuna chochote kinachoendelea.

Tumeona baadhi ya timu nyingi zikipanda Ligi Kuu kwa sababu kama hizo, tena kwa mbwembwe nyingi, lakini zikifika Ligi Kuu zinatelekezwa na kuanza kulia njaa.

Mashabiki wengi wa soka nchini wanapenda zaidi timu zenye uchumi mzuri ndiyo zipande, ili ziende kuleta chachu na ushindani wa kweli ili ligi iwe ngumu, isiyotabirika na isiyokuwa na timu dhaifu kwa sababu tu ya uchumi.

Ndiyo maana wengi walitaka Gwambina FC ipande kwa sababu inaonekana kuwa iko vizuri kiuchumi. Ni timu ambayo tangu iko Ligi Daraja la Kwanza ilionekana kabisa haina njaa.

Kwenye Kundi A, mashabiki wengi wa soka walionekana kuipigia debe zaidi Ihefu FC ipande kwa sababu tu imeonekana kuwa na uchumi mzuri kutokana na kumilikiwa na wakulima wakubwa wa mpunga, wakichanganyika na wafanyabiashara wa zao hilo.

Kwa bahati mbaya sana, Ihefu imeangukia kwenye mechi za mchujo na Dodoma Jiji FC imepanda kwa nguvu zake na uwezo wa wachezaji wake.

Sasa ili kuwathibitishia mashabiki kuwa hajaipandisha timu hiyo kisiasa, viongozi wa jiji hilo baada ya kumaliza kushangilia wajue wana jukumu zito la kuitunza timu hiyo, kuingia mifukoni, kusaka wadhamini na kutafuta pesa za kusajili wachezaji wazuri, wazoefu na wenye uwezo wa kupambana katika Ligi Kuu.

Hatutarajii timu ya Dodoma Jiji baada ya kupanda, basi waachiwe tu viongozi wa timu pekee, baadaye waanze kulia njaa na kutembeza bakuli kwa wananchi na wabunge.

Hii itakuwa ni aibu, na baadhi ya mashabiki wa soka wataanza kuhoji nguvu zilizotumika kuipandisha timu hiyo, halafu inaachwa ikiwa hoi.

Tunaitaka Dodoma Jiji FC iwe na makali, uwezo na wachezaji wenye uwezo wa hali ya juu, pamoja na uchumi usiotetereka kama ilivyokuwa timu za Waziri Mkuu na CDA.

# Wagombea wa CHADEMA waonywa rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAGOMBEA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wamekumbushwa kuzingatia mwongozo wa chama chao dhidi ya vitendo vya rushwa.

Katibu wa CHADEMA Jimbo la Kibaha Mjini, Michael Nkobi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kufunga uchukuaji na kurejesha fomu za kugombea bafasi ya ubunge katika jimbo hilo.

Nkobi alisema chama hakitasita kuwachukulia hatua kwa watakaobainika kijihusisha na vitendo vya rushwa na kukiuka kanuni na taratibu za kampeni.

"Hatutasita kuchukua hatua kwa taarifa za rushwa na atakayebainika kukiuka kanuni na miongozo ya chama chetu na kanuni za kampeni zitakapokiukwa," alisema Nkobi. Akirudisha fomu ya kuomba kuchaguliwa kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba Michael Mtally katika Jimbo la Kibaha Mjini, alisema amelazimika kuchukua fomu kwa mara nyingine kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuongeza Jimbo la Kibaha kutokana na hali ya maendeleo kutoendana na kasi ya Rais Magufuli.

Mtally alisema, endapo atapitishwa na chama chake na wananchi, ana mipango ya kuwashirikisha wananchi katika kuibua miradi ya maendeleo ambayo itakuwa mkombozi wa wananchi.

"Nitajikita zaidi kuongeza vyumba vya madarasa, ujenzi wa zahanati na kuboresha huduma za afya hususani kwa wazee ambao wanatakiwa kutibiwa bure pamoja na kuhakikisha dawa zinapatikana kwa urahisi kuondoa usumbufu kwa kundi hilo," alisema Mtally.

Nae Mery Muro ambaye amemaliza muda wake wa Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Chama hicho, alisema, kwa kipindi cha miaka mitano ameyafahamu vizuri mahitaji ya wananchi hivyo amechukua fomu ya kuomba kuchaguliwa kugombea Jimbo la Kibaha Mjini na Viti Maalum kushughulikia matatizo aliyoyabaini.

Mwenyekiti wa Jimbo la Kibaha, Moses Mgae, alisema chama hicho kimejipanga kuchukua nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa itapitisha wagombea wenye uwezo na wanaokidhi kuongeza wananchi.

# EPZA inavyowasaidia wakulima soko la malighafi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum ya Uwekezaji na Mauzo Nje ya Nchi (EPZA), imesaidia kuwaunganisha wakulima kuuza malighafi katika viwanda na kuwahakikishia soko la uhakika na ongezeko la kipato kutoka kwenye mazao yao.

Meneja wa EPZA, Grace Lemunge, alipokuwa anaongea kuhusu ushiriki wao katika maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere katika Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

"Tumepiga hatua kubwa sana katika kuwapa wakulima taarifa muhimu pamoja na kuwaunganisha na wenye viwanda ambavyo vipo chini ya EPZA na hili limewasaidia sana katika kupata masoko ya uhakika na ongezeko la kipato," alisema.

Alisema washiriki na wageni waliotembelea maonyesho ya mwaka huu, wana kwenda kwa wingi katika banda lao Sabasaba ili kupata maelezo ya kunufaika na motisha unaotolewa na mamlaka ya EPZA.

Lemunge alisema maonyesho hayo ni fursa muhimu ya kuwahabarisha wananchi na wakulima na wajasiriamali ili kuwaunganisha na masoko hasa viwanda ambavyo hutumia malighali ya kilimo.

EPZA imetumia maonyesho ya mwaka huu kuwaunganisha wakulima wa maparachichi na kiwanda kipya kilichopo mkoani Arusha kinachofanya kazi chini ya mwamvuli wa EPZA na kuwaongezea fursa kubwa ya soko la uhakika na kipato.

Mamlaka imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na viwanda vinavyoongeza thamani mazao kama vile dengu, choroko na mbaazi ambavyo huuzwa katika masoko ya India na ya Asia.

Pia, EPZA imefanya kazi kwa karibu na wakulima wa ufuta na kuwaunganisha na wanunuzi ambao huuza katika masoko ya Asia na Ulaya.

Meneja Uhamasishaji Uwekezaji alisema katika maonyesho ya mwaka huu viwanda 16 vilivyo chini ya mwamvuli wa EPZA vimeshiriki na kuwahabarisha washiriki na wageni waliotembelea maonyesho hayo.

Baadhi ya viwanda hivyo ni DZ Cards ambacho kinashughulika na utengenezaji wa kadi za kieletroniki ili kurahisisha kufanya ununuzi wa bidhaa.

Kiwanda kingine ni Tooku Garments Co., Limited kinachozalisha nguo kwa ajili ya kuuza katika soko la Marekani.

Viwanda hivi vimekuwa chachu kubwa kutoa ajira kwa Watanzania wengi pamoja na kuchangia pato la taifa kupitia kodi mbalimbali.




Ofisa Msimamizi Misaada wa Taasisi ya Kiislam ya Direct Aid, Saleh Haruna Saleh (kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa Athman Said, mkazi wa Kata ya Mbwera, Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, ambaye ni mmoja wa waathirika wa mafuriko. Taasisi hiyo imetoa tani 15 za vyakula kwa ajili ya kusaidia kaya 1,800 zilizoathirika juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri Mpango kuongoza mkutano mawaziri SADC

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kuongoza mkutano wa mawaziri wanaohusika na masuala ya fedha na uwekezaji wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jopo la Mapitio ya Uchumi Mpana, unaotarajiwa kufanyika Jumatano kwa njia ya mtandao katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini, Benny Mwaipaja, ilisema mkutano huo utatanguliwa na kikao cha Makatibu Wakuu wa Wizara za Fedha na Benki Kuu wa SADC, utakaofanyika kwa siku mbili kuanzia leo.

Taarifa ilisema mkutano huo utawakutanisha mawaziri wenye dhamana na masuala ya fedha na uwekezaji na Magavana wa Benki Kuu kutoka nchi 16 wanachama wa SADC na utajadili masuala ya fedha na uwekezaji pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji katika mkutano uliofanyika mwezi Julai 2019, Windhoek, Namibia.

Vilevile, mkutano huo utajadili na kutoa maamuzi ya kisera kuhusu athari za kiuchumi na kijamii za Covid-19.

Mkutano huo ulipangwa kufanyika ana kwa ana kuanzia Julai 13-17, 2020, lakini kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, utafanyika kwa njia ya mtandao kuanzia leo hadi Jumatano.

Taarifa ilieleza mkutano huo ni utekelezaji wa maelekezo ya mkutano wa dharura wa Baraza la Mawaziri wa SADC uliofanyika Machi 18 2020, jijini Dar es Salaam, ambao ulimwelekeza Mwenyekiti wa Baraza kwa kushirikiana na Sekretarieti ya SADC kusimamia zuio la kufanyika kwa mikutano ya ana kwa ana kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo.

# Ujenzi Ikulu ya Chamwino kukamilika ndani ya miezi 6

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, amesema ujenzi wa Ikulu mpya ya Chamwino unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita kuanzia sasa, huku akisisitiza inajengwa na Watanzania.

Hata hivyo, amesema kuna baadhi ya nchi zilizokuwa zimejipanga kujenga Ikulu hiyo, lakini alizikatalia na kuona ni dharau.

Sambamba na hilo, amesema anafahamu urais na uenyekiti ni kazi kubwa na yenye majukumu mengi, lakini ina matusi na mateso.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye halfa ya chakula cha mchana kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM waliotembelea kuangalia ujenzi huo, Rais Magufuli alisema Ikulu hiyo ni kubwa kuliko zote duniani.

"Ikulu hii ni kubwa kushinda Ikulu yoyote duniani, wakati tumeamua kuhamia hapa zipo nchi mbalimbali zilijipanga kutujengea Ikulu nikasema hii ni dharau, ukimruhusu jirani hadi akutandikie kitanda chako cha kulala nyumbani kwako siku nyingine atafanya maajabu."

"Au akujengee nyumba, atajua hichi chumba cha kulala wewe, cha watoto, au jirani awe na nguvu nyingi, ujue hapo familia yako haipo, yule jamaa atarudi kinyume nyume akishindwa kuchukua mke wako atachukua binti zako, ndio maana nikasema Ikulu hii itajengwa na Watanzania wenyewe," alisema.

Aliwaambia wanachama na Watanzania kuwa Ikulu hiyo ni yao, na yeye ni mpangaji ndio sababu amevialika na vyama vingine vya siasa kwa kutambua kwamba wanapaswa kujenga Tanzania moja.

"Hii Ikulu inajengwa na Watanzania vijana wetu wa JKT na Mkuu wa JKT Meja Jenerali Mbuge amenihakikishia ndani ya miezi sita, Ikulu yote itakuwa imekamilika...tutakuwa na Ikulu mpya mfano wa ile ya Dar es Salaam, huku ndiko kujitegemea, huu ndio uzalendo na huu ni Utanzania," alieleza.

Kuhusu maboresho ya Jiji la Dodoma, Rais Magufuli alisema Sh. bilioni 600 zimetengwa kujenga barabara za mzunguko za njia nne huku Sh. bilioni 500 zikitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato.

"Nimeifanya hii kazi kwa sababu ya nguvu zenu na msaada wa Mungu, nawashukuru wana-CCM wote, Watanzania wa vyama vyote kwa jinsi walivyotoa ushirikiano mkubwa kwa miaka mitano iliyopita."

"Nivipongeze na kuvishukuru vyombo vya ulinzi na usalama wamefanya kazi nzuri sana msione vya elea vimeundwa, wamefanya kazi kubwa kule Kibiti na Rufiji ndugu zetu askari zaidi ya 20 walipoteza maisha," alisema.

Awali, mgombea urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisema kwa sasa anakwenda kupambana na vyama vya upinzani akishirikiana na waliokuwa wakigombea nafasi hiyo, viongozi wa chama Zanzibar, wanachama wa CCM ambapo wamemhakikishia wanakwenda kushinda uchaguzi wa Zanzibar.

Naye Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alisema sasa ni wakati wa kuungana, nguvu iwe moja kufanya kampeni na CCM iibuke na ushindi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha UDP, John Cheyo, alisema chama chake kinamuunga mkono Rais Magufuli katika uchaguzi wa Oktoba mwaka huu.

"Nawashangaa wanaojiita wapinzani ambao wanatembea Ulaya, Amerika wakiponda nchi tamu kama Tanzania, chini ya uongozi wa Rais Magufuli, kweli watu wa CCM mnapaswa kujivuna kuwa na Mwenyekiti kama Magufuli," alisema.

Aliongeza: "Nawaonea huruma watakaompinga Magufuli, ngoma imeshamalizika, UDP tunawaomba angalau tupate diwani hata mmoja, wabunge wawili. Hakuna chama kilichoandikwa kwenda kukiondoa CCM, kama una wazo hilo futa kabisa. Tuungane kwenda kuiondoa CCM halafu uweke nini?"

Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, alisema wanaopongeza Tanzania kuingia uchumi wa kati ni wagonjwa wa akili.

Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, alisema ujenzi wa Ikulu hiyo ni heshima kwa nchi.

"Nataka tuondoke hapa na neno moja la umoja, tufute tofauti, tuziweke pembeni, tuungane tuwe na kazi moja kumtoa mpinzani kwenye jimbo...muda wa tofauti umekwisha naamini tukiondoka kwa umoja, utabaki Ikulu, mikoani tutakufanyia kazi," alisema.

## Kampuni yaonywa kusuasua utekelezaji wa mradi wa umeme

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, ameinyooshea kidole kampuni ya ukandarasi ya Namis inayotekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijijini vilivyopo pembezoni mwa mji (Peri Urban) Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, na Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam kwa kusuasua kutekeleza mradi huo.

Ameiagiza kuongeza kasi hadi kufikia mwishoni mwa Agosti, 2020 iwe imekamilisha kazi ya utekelezaji wa mradi huo.

Mhandisi Masanja alisema hayo Jumamosi wilayani Kisarawe mkoani Pwani wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaotekelezwa kwa kasi isiyoridhisha, ikilinganishwa na makubaliano na matakwa ya mkataba husika, huku mkandarasi akieleza sababu zisizokubalika zinazochangia kusuasua kwa mradi huo.

Mhandisi Masanja alieleza kuwa kwa sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 39, ambayo ni tathmini ya chini na makubiliano ya mkataba yanayoelekeza kuwa tangu kusainia kwa mkataba huo na kuanza kwa utekelezaji wa mradi Desemba, 2019, hadi kufikia sasa mradi huo ulitakiwa kuwa umekamilika kwa asilimia 77.

Aidha, alimtaka mkandarasi huyo kuongeza nguvu kazi na magenge ya watu watakaofanya kazi usiku na mchana ili kwenda sambamba na kasi ya utekelezaji wa mradi huo, ili ukamilike ndani ya muda uliopangwa.




Mkuu wa Gereza la Musoma, Aliko Mwakalobo (wa pili kulia), akishuhudia mshindi wa bahati nasibu ya Tusua Mapene, Sajenti Celestine Kalemezi (katikati), akipongezwa na Meneja Mauzo wa Vodacom Tanzania PLC-Musoma, Jovinth Ikate, baada ya kuibuka mshindi wa Sh. milioni 128. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanisa laipongeza serikali nchi kuingia uchumi wa kati

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

SERIKALI ya Rais John Magufuli imepongezwa na Kanisa Katoliki kwa juhudi zake zilizofanikisha kufikia uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025, ndilo lengo lililokuwa limewekwa na serikali.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, ambaye pia ni msimamizi wa Kitume wa Jimbo Katoliki la Bunda, Askofu Renatus Nkwande, kwenye Ibada ya misa Takatifu ya kupewa Daraja Takatifu la Upadri Shemasi Thobias Mwanisawa, iliyofanyika kwenye viwanja vya kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo Parokia ya Bunda, ndiko makao makuu ya Jimbo la Bunda.

Askofu Nkwande alisema Serikali ya Rais Magufuli inapaswa kupongezwa kwa juhudi za kufikia katika uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025, na kwamba tuendelee kudumisha amani iliyopo nchini kwa kuwa ndiyo iliyoifikisha Tanzania katika hatua hiyo. "Naipongeza serikali yetu kwa juhudi za taifa letu kufikia uchumi wa kati kwa sababu hii ni fahari ya nchi nzima," alisema Askofu Nkwande.

Aidha, Askofu Nkewande alisema kuwa kanisa hilo linaombea uchaguzi mkuu ujao ufanyike kwa amani, utulivu na haki, ambapo pia amewaomba watu waache kushabikia makundi ambayo yanahamasisha vurugu.

"Pia tuendelee kudumisha amani tuliyonayo, kwani ndiyo imetufikisha katika hatua ya uchumi wa kati. Ninawaomba watu waache ushabiki wenye fujo katika vyama vya siasa na pia waache kushabikia makundi yanayohamasisha vurugu na pia wapuuze ajenda ya kuleta vurugu.

"Lakini tuiombee nchi yetu na viongozi wote katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi ili tuweze kufika salama na kupata mafanikio," alisema Askofu Nkwande.

Kwa upande wake Padri aliyepewa daraja la upadri, Thobias Mwanisawa, alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumfikisha katika hatua hiyo, pia amewaomba vijana kuitikia wito.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Janeth Mayanja, alisema serikali na madhehebu ya dini wanauhusiano mkubwa na mzuri.

HABARI KITAIFA

# Kibano kwa shule binafsi chaja

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imewaagiza wathibiti ubora wa shule, kufanya uhakiki na ukaguzi wa kina kwa shule binafsi kama zinaendelea kufuata miongozo inayokidhi vigezo vilivyowekwa.

Miongozi mwa vigezo hivyo ni kuwa na walimu wenye sifa na mikataba, majengo na kuwapo kwa bodi na kamati za shule na endapo zitabainika zina mapungufu hayo, zifungwe.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, wakati akifunga mafunzo kwa watumishi wapya wa udhibiti ubora wa shule nchini katika Chuo cha Ualimu Kigurunyembe mkoani hapa.

Alisema wapo baadhi ya wamiliki wa shule binafsi wamekuwa wakikiuka maagizo na miongozi ya uendeshaji wa shule hizo kutokana na dharau na ujeuri wa pesa, hali ambayo wakati mwingine inasababisha kushindwa kutoa elimu iliyokusudiwa huku lawama zikiangukia serikali.

"Wapo baadhi ya wamiliki wa shule binafsi wanaleta dharau kwa serikali kwa sababu wamejenga majengo yao...wao wana majengo, lakini wajitambue kuwa majengo ni mali yao na shule ni mali ya serikali hivyo wanapaswa kufuata taratibu zote zilizowekwa ikiwamo kuwa na kamati na bodi za shule pamoja na walimu wenye sifa," alisema.

Alisema hatua ya kupitia shule hizo na kuona kama bado zinakidhi vigezo ni kutaka kusaidia watambue nafasi zao katika kuhakikisha wanatoa elimu iliyo bora na yenye kukidhi viwango vinavyokubalika ili kutatua changamoto ya elimu nchini.

Hata hivyo Dk. Akwilapo aliwaonya wadhibiti ubora kutojihusisha na vitendo vya rushwa kwa nia ya kuzikingia kifua shule hizo binafsi na badala yake atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo hatua kali zitachukuliwe ikiwamo kufukuzwa kazi.

"Hii ni serikali inayopiga vita kwa nguvu vitendo vya rushwa... yeyote yule kati yenu wadhibiti ubora atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo katika ukaguzi hatutasita kuchukua hatua kali dhidi yake ikiwamo kuondolewa kazini." Alisema idara hiyo ni miongoni mwa idara zinazotajwa kujihusisha na vitendo vya rushwa hasa wanapofanya ukaguzi katika shule zinazomilikiwa na sekta binafsi, hivyo kuhakikisha wanafanya kazi yao kwa kuzingatia maadili na viapo vyao.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Avemaria Semakafu, alisisitiza umuhimu wa wadhibiti ubora kuzingatia mavazi yenye maadili ya utumishi wa umma pamoja na kufuata miongozi wakati wa kutekeleza majukumu yao kwa kuwa wao ni watu muhimu katika maendeleo ya elimu nchini.

Aliwataka watumishi hao kuzingatia suala la utunzaji wa kumbukumbu pamoja na nyaraka za serikali kuacha kuzisambaza kwenye mitandao ya kijamii, na atakayebainika kufanya hivyo sheria itachukua mkondo wake.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu (kushoto), akizungumza na wananchi wa eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa usafi wa mtaro wa maji machafu unaosafishwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) katika kufanikisha mkakati wake wa utunzaji wa mazingira. (Kulia) ni Mkurugenzi wa Ufundi na Uzalishaji wa kampuni hiyo, Richmond Raymond.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yaokoa fedha, mali za bil. 1.5/-

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, imeokoa jumla ya Sh. 1,485,393,287 zikiwamo mali na fedha.

Miongoni mwa mali hizo ni maghala mawili ya kuhifadhia mazao mbalimbali kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Mkuu wa taasisi hiyo mkoani humo, Stepen Chami, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na wanahabari kuhusiana na kazi iliyofanywa na watumishi wa taasisi hiyo. Amesema fedha na maghala yaliyookolewa yapo katika Wilaya ya Nachingwea kuanzia Aprili hadi Juni 30, mwaka huu, zikijumuisha fedha za wakulima wa korosho na ufuta.

Chami alisema Sh. 1,203,393,287 zinahusisha malipo ya wakulima wa korosho na ufuta.

Mkuu huyo wa TAKUKURU Lindi alisema katika kipindi hicho pia taasisi hiyo imeweza kurejesha katika umiliki wa Serikali maghala mawili ya kuhifadhia mazao yenye thamani ya Sh. 282,000,000, na kufanya Jumla ya fedha zilizookolewa na taasisi hiyo kufikia Jumla ya Sh. 1,485,393,287. Alisema urejeshaji wa maghala hayo mawili mikononi mwa serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea itaweza kupata jumla ya Sh. 114,000,000 zitakazotokana na utunzaji wa zao la ufuta pekee msimu wa fedha 2020/2021.

Pia, alisema kwamba katika kipindi hicho, taasisi hiyo imerejesha kurejesha umiliki wa wananchi trekta moja na viwanja viwili ambavyo wajanja waliokuwa wamejimilikisha.

## TFS yaanzisha shamba la mianzi kwa majaribio

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umeanzisha shamba la mianzi kwa ajili ya majaribio katika msitu wa Ruvu Kaskazini mkoani Pwani.

Akitoa maelezo kuhusu lengo la kuanzisha shamba hilo kwa wananchi waliotembelea banda la TFS katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya 44, Meneja wa shamba hilo, Furtunate Senya, alisema lengo ni kuhakikisha kwamba bidhaa za mianzi zinapatikana kwa wingi kwa ajili ya viwanda.

Alisema kuanzisha viwanda vinavyotumia malighafi ya mianzi kutatoa fursa kwa wananchi wengi kupata kipato na ajira.

"Tuna bidhaa mbalimbali zinazotokana na mianzi na tumekuja Sabasaba kuwaonyesha na kuwafundisha faida na fursa mbalimbali zinazotokana na bidhaa hizi, watu ni wengi wanakuja kujifunza na wamevutiwa kuwa na biashara zinazotokana na mianzi hii, haya ndiyo tunayotaka," alisema Senya.

"Mbali na pombe ambayo inapatikana kutokana na miti hii ya ulanzi, lakini kuna fursa nyingine inayotokana na miti hii ikiwamo vijiti vya kuchokonolea uchafu kwenye meno na hata vijiti vya kuchomea mishikaki ya nyama. Kwa hiyo hii ni fursa nzuri ambayo wananchi wanatakiwa kuichangamkia na ikawaletea kipato."

Mmoja wa watu waliotembelea katika banda hilo ambaye ni Diwani wa Kata ya Mseke mkoani Iringa, Robert Lawa alisema wananchi katika eneo lake wamekuwa wakipata kipato kutokana na miti hiyo ya ulanzi.

"Kwa kweli naweza kushuhudia kwa ujasiri kabisa kwamba ulanzi imewakomboa watu wengi mkoani Iringa na hata walio katika eneo langu, watu wanasomesha watoto na kuendesha maisha yao kutokana na ulanzi, kwa hiyo ikiboreshwa zaidi na kupeleka viwandani, watu wengi watafaidika," alisema Lawa.

# Wazazi wa watoto waliofanyiwa ukatili wasaidiwa kujitegemea

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

WAZAZI wa watoto waliofanyiwa vitendo vya udhalilishaji wametakiwa kuitumia fursa ya ufugaji wa kuku kuzalisha ili kuwasaidia kujikimu kiuchumi.

Akizungumza na wazazi hao kwenye mafunzo ya ufugaji wa kuku Mkanjuni Chakechake, Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) -Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema wamepanga kuwapatia vifaranga baada ya mafunzo ili kuwawezesha kiuchumi.

Alisema ni vyema wazazi hao kuitumia fursa hiyo kuzalisha zaidi ili kuwasaidia kujiendeleza kiuchumi.

"Tunawapa mafunzo ya ufugaji na tutawapa vifaranga baada ya kukamilisha kujenga mabanda ya kufugia, hiyo ni fursa adhimu kwenu, muifanye kwa moyo mkunjufu, itawasaidia kuwakwamua na maisha magumu," alisema.

"Tumebaini kwamba sababu kubwa ya kuwapo kwa wimbi la udhalilishaji katika jamii chanzo chake ni mifarakano ya kifamilia na utelekezaji, hivyo TAMWA imeamua kuandaa mafunzo haya ili yawasaidie waathirika wa vitendo hivyo kujishughulisha katika mambo za kiuchumi," alisema.

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo, Omar Hamad Mjaka, alisema, mafunzo hayo yamejikita kuwapatia mbinu mpya za ufugaji wa kisasa kinamama hao ili kuwasaidia kimaisha.

Mmoja wa washiriki aliishukuru TAMWA kwa kuwezesha mafunzo hayo, na kwamba yatawasaidia kujikwamua kiuchumi kutokana na hali ngumu ya maisha waliyonayo.

Mafunzo hayo ni utekelezaji wa mradi wa Jukwaa la Wanahabari la Kumaliza Udhalilishaji Zanzibar, unaotekelezwa TAMWA Zanzibar kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA).

# Tani milioni 2 za kuku kupungua ifikapo 2030

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

SERIKALI inaendelea kuwapatia mafunzo wafugaji wa kuku ili waweze kuzalisha idadi kubwa ya mifugo hiyo.

Imeelezwa kuwa kama wafugaji wa kuku watashindwa kufanya uwekezaji wa nyama nyeupe hali hiyo itasababisha kupungua kwa nyama nyeupe tani milioni mbili ifikapo mwaka 2030.

Hayo yalisema na Mkurugenzi Uzalishaji Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Adam Nandonde, walipokuwa wanawapatia mafunzo wafugaji wa kuku kutoka makundi 30 wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

"Tumetoa mafunzo ya siku mbili kwa wafugaji kuku kutoka makundi 30 ambayo yanafuga kuku," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imeandaa mpango kabambe wa mifugo wa mwaka 2017/2021 ambapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi zinausimamia mpango huo.

Alisema mpaka kufikia mwaka 2030 watahakikisha nyama nyeupe inapatikana kwa wingi.

"Bila kuwapo na elimu ya ufugaji ifikapo mwaka 2030, nyama nyeupe haitakuwapo na kutakuwa na upungufu wa nyama," alisema. Aliongeza kuwa wizara imeanza uzalishaji wa dawa na chanjo ili kuwasaidia wafugaji kuitumia katika mifugo yao pale itakapokumbwa na magonjwa ya mdondo.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, aliwataka wafugaji waliopatiwa mafunzo ikiwamo kukabidhiwa vifaranga kila kikundi kuku 42 pamoja na kuwataka mafunzo hayo wayatumie vizuri ili yawasaidie kuzalisha kuku wenye ubora.

Kwa mujibu wa Nandonde, mikoa iliyobahatika na mafunzo na kupatiwa vifaranga kupitia serikali ni Singida, Dodoma, Dar es Salaam, Lindi na Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.



Mkuu wa Idara ya Huduma za Kifedha kwa Biashara za Kimataifa Benki ya NMB, Linda Teggisa (kushoto), akizungumza wakati mabalozi wa nchi nane wanaoziwakilisha nchi zao nchini, walipotembelea banda hilo kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushirikishaji wazawa miradi ya kimkakati wahimizwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imesema inaupa uwezeshaji na ushirikishaji wazawa kipaumbele katika kuchangia kwake utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini hasa endelevu ya kimkakati iliyoanzishwa na Serikali ya Rais John Magufuli.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Idara ya Huduma za Kifedha kwa biashara za kimataifa, Linda Teggisa, mwishoni wa wiki wakati akitoa ufafanuzi baada ya kuupokea ujumbe mzito wa mabalozi nane walioambatana na uongozi wa Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) walipotembelea banda la Benki ya NMB kwenye Maonyesho ya Sabasaba.

Teggisa aliufahamisha ugeni kwamba pamoja na kuwahudumia wageni wanapokuja Tanzania kuwekeza na kushiriki katika miradi mbalimbali, maendeleo ya wazawa yanapewa kipaumbele kikubwa na benki yao.

Alisema suala la kuwawezesha Watanzania ili washiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali na mikubwa ni la msingi sana kwa benki hiyo inayojivunia kuwa na rasilimali zenye thamani ya takribani Sh. trilioni 6.5 pamoja na amana zipatazo Sh. trilioni 4.7, huku ikiwa na matawi 225 nchi nzima ambayo yanapatikana kwenye asilimia 98 ya wilaya zote nchini.

"Kwetu sisi kama benki, suala la 'local content' (uwezeshaji na ushirikishaji wazawa) ni muhimu na la msingi," Teggisa alisisitiza kuhusu jinsi benki hiyo inavyoshiriki kwenye utekelezaji wa vipaumbele vya kiuchumi na maendeleo vya uongozi wa Rais Magufuli unaozingatia kuwapa nafasi kubwa Watanzania kwenye utekelezaji wa miradi mingi.

"Kwa ufupi sisi kama benki kubwa nchini tunatoa huduma za kifedha ambazo zinahusisha sekta mbalimbali na miradi nyeti kama sekta ya kilimo, uchukuzi, nishati, maendeleo ya miundombinu pamoja na zile za afya na elimu," aliongeza na kusema kwamba mfano mzuri wa uwezeshaji wa wazawa ni wa makandarasi wa humu nchini.

Aliwaambia mabalozi hao wakiwamo wanaotoka kwenye baadhi ya nchi ambazo kampuni zao zinashiriki katika kutekeleza miradi ya kimkakati kuwa benki yao ina jukumu la kuwahudumia wenyeji, lakini kuhakikisha kuwa wafanyabiashara na wawekezaji wa nje nao wananufaika na huduma zao bora za rejareja na za wateja makubwa.

Teggisa alifafanua jinsi NMB inavyoshiriki katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kwa kumsaidia mkandarasi mkuu wa mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), kampuni ya Yapi Merkezi ya Uturuki ambayo balozi wake nchini alikuwa kwenye msafara wa TCCIA uliotembelea banda la benki hiyo.

Mabalozi wengine walioshuhudia ushiriki wa Benki ya NMB ni kutoka Misri, Pakistani, Kenya, Uganda, Falme za Nchi za Kiarabu na Sweden.

# Nipashe Spotika



NDOTO MBAYA KWA CITY, JUVENTUS NA BAYERN UK. 12&13



# FERNANDES MFALME ALIYEIFUFUA UNITED

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Bruno Fernandes ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwezi wa Ligi Kuu England kwa mara ya pili mfululizo.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno, alionyesha kiwango cha kuvutia mno kwa kipindi cha Juni na hivyo kujikuta akiibeba tena tuzo hiyo baada ya kufanya hivyo Mei, mwaka huu.

Bruno ametoa mchango mkubwa zaidi kwa mechi za hivi karibuni za United ambayo inaonekana kama 'imefufuka' upya na hivyo kujiweka kwenye mazingira mazuri zaidi ya kutoa changamoto kubwa katika mbio za ubingwa kuelekea msimu ujao wa 2020/21.

Kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer kilionekana kutokuwa kwenye makali yake mwanzoni mwa msimu huu, lakini baada ya kumwongeza Fernandes, wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari akitokea Sporting CP, kumesaidia 'kufufuka' kwa kiwango cha timu hiyo.

Sasa timu hiyo inaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kupambana kupata nafasi ya kufuzu kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Bao lake na pasi ya mwisho dhidi ya Aston Villa Alhamisi iliyopita, lilimfanya afikishe mabao saba kwenye ligi na 'asisti' sita katika mechi 10 tu za ligi hiyo alizocheza hadi sasa.

Hii ni moja ya takwimu bora zao kwake kwa kuanza kucheza kwenye Ligi Kuu England katika maisha yake ya soka hadi sasa.

Uwepo wake dimbani umeonekana kuwa na mchango mkubwa kwa timu na ameweza kuisaidia zaidi safu ya ushambuliaji ya timu hiyo. Juni, United ilianza kwa kuifuata Tottenham Hotspur, ambako walianza kwa kufungwa kabla ya Fernandes kusawazisha mambo na kuwawezesha kuondoka na pointi muhimu.

Halafu wakafuatiwa na ushindi mtamu wa mabao 3-0 dhidi ya Sheffield United ambapo Fernandes alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwenye mchezo huo kwa kusaidia upatikanaji wa mabao hayo.

Baada ya hapo akafanya yake kwenye mchezo dhidi ya Brighton kwa kutikisa nyavu mara mbili.

Alimaliza mwezi huo akiwa na mabao matatu katika mechi tatu alizocheza na kuingiza kwenye mbio za kuwania tuzo.

Katika orodha ya wachezaji sita iliyotolewa kuwania tuzo hiyo, ilimjumuisha pia mchezaji mwenzake pale United, Anthony Martial, nyota wa Southampton, Danny Ings, wakali wa Wolves, Raul Jimenez na Conor Coady, pamoja na nyota mwenye kiwango cha kuvutia kwa sasa wa Newcastle, Mfaransa Allan Saint-Maximin.


Na mwisho wa siku Mreno huyo ndiye akaibuka mshindi kwa kuibeba kwa mara ya pili mfululizo. Fernandes na United wataendelea kutamba kwenye ligi hiyo, wakati leo Jutamatu watakuwa ugenini kuwavaa Southampton.

Wanakwenda kwenye mchezo huo wakijua wazi ushindi utawasukuma na kuwafanya wabakize pointi tatu kufika kwenye hatua ya kufuzu michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Hii ni kutokana na wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City ambao wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, kukabiliwa na adhabu ya kufungiwa kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu ujao.

## ISIKUPITE

REAL Madrid imemweleza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Paris St-Germain, Kylian Mbappe, ambaye ana umri wa miaka 21, asisaini mkataba mpya na klabu hiyo ili iwe rahisi katika kukamilisha mchakato wa kumsajili ifikapo majira ya joto mwakani.



LIGI YA MABINGWA ULAYA

# NDOTO MBAYA KWA MAN CITY, JUVENTUS NA BAYERN



LEWANDOSKI

**LISBON,** Ureno

DROO ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali imeshapangwa, na inaonyesha kutakuwa na mnyukano mkali baina ya timu vigogo kwenye michuano hiyo.

**Michuano hiyo ililazimika kusimama kutokana na dunia kukumbwa na mlipuko wa virusi vya corona, na hivyo sasa itaendelea na kukamilika kuanzia Agosti, mwaka huu.**

Kutokana na muda, mashindano hayo kuanzia kwenye hatua ya robo fainali yatachezwa kwa mtindo wa mechi moja tu bila marudiano na zitachezwa katika kituo kimoja cha jijini, Lisbon nchini Ureno.

Makala hii inaangalia namna miamba ya Ulaya itakavyotifuana kuhakikisha mwisho wa siku mmoja wao anaondoka na taji hilo kubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya.

### VIGOGO

Barcelona na Bayern Munich zitakutana kwenye robo fainali kama zote zitafanikiwa kushinda kwenye mechi zao zilizobaki. Timu hizo mbili zimebakiwa na mchezo mmoja mmoja ili kufuzu hatua hiyo.

Timu zote mbili hizo zinahitaji kumalizia mechi zao za pili kwenye hatua ya mtoano wa timu 16, huku Bayern inaonekana ni kama imetanguliza mguu wake mmoja mbele.

Kwani kwenye mchezo wake wa kwanza ugenini ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Chelsea, huku Barcelona watawakaribisha Napoli baada ya kutoka sare ya kufungana 1-1 mchezo uliopigwa nchini Itallia.

Wao Manchester City kama wataweza kumaliza kazi waliyoianza kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16 bora dhidi ya Real Madrid, kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kitafuzu robo fainali na kitakutana kati ya Juventus au Lyon.

City ilishinda mabao 2-1 kwenye mchezo wake wa kwanza jijini Madrid uliopigwa Machi, mwaka huu, huku Juventus watalazimika kipindua kichapo cha bao 1-0 walichokipata kwenye mchezo wa kwanza kutoka kwa Lyon, kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 bora.

Baada ya kusimamishwa kwa michuano hiyo Machi, kutokana na mlipuko huo wa corona, mechi zote zilizobaki za hatua ya timu 16 zitachezwa kwa siku mbili tu, Agosti 7 na 8, mwaka huu.

Washindi watasonga mbele kwenye hatua ya timu nane (robo fainali), ambapo zitafanyika Lisbon.

Droo hiyo imeibua uwezekano wa kushuhudia mchezo wa Clasico kwenye nusu fainali, kwani Barcelona na Madrid wakishinda mechi zao hatua ya robo fainali, maana yake watakutana kwenye nne bora za mwisho kutafuta nafasi ya kufuzu fainali.

Kwa upande mwingine droo hiyo, RB Leipzig ya Ujerumani ambayo imefuzu hatua hiyo kwa mara ya kwanza itakutana na Atletico Madrid, ambao walifungwa na Real Madrid kwenye fainali ya mashindano hayo ya mwaka 2014 iliyopigwa huko Lisbon 2014.

Atletico walitinga hatua hiyo baada ya kumtoa bingwa mtetezi wa mashindano hayo, Liverpool hatua ya mtoano wa timu 16.

Mshindi wa Leipzig dhidi ya Atletico atakutana na kati ya Paris Saint-Germain au Atalanta kwenye hatua ya nusu fainali.

Robo fainali hiyo itachezwa kati ya Agosti 12 na 15, mwaka huu kwenye mji huo mkuu wa Ureno, huku mechi hizo zikichezwa katika viwanja viwili, Estadio da Luz kinachomilikiwa na klabu ya Benfica na Estadio Jose Alvalade kinachomilikiwa na Sporting.

Kwa upande wa nusu fainali imepangwa kupigwa kati ya Agosti 18 na 19, na fainali yake itapigwa Agosti 23 kwenye dimba la Estadio da Luz.

Mehi zote hizi zitachezwa wakati milango ikiwa imefungwa kutoruhusu mashabiki, baada ya shirikisho la soka la Ulaya, Uefa, kuthibitisha Alhamisi kwamba "mechi zote zitatakiwa kuchezwa huku milango ikiwa imefungwa hadi itakavyotaarifiwa vinginevyo" kutokana na wasiwasi wa hali ya usalama wa afya barani Ulaya.

Hali jinsi ilivyo jijini Lisbon bado kuna vizuizi vya watu kukusanyika na pia kuna maeneo watu hawaruhusiwa kutoka nje, kwa sababu idadi ya maambukizi ya virusi vya corona, inazidi kuripotiwa kila siku.

### RATIBA KAMILI

Real Madrid au Manchester City v Olympique Lyon au Juventus
RB Leipzig v Atletico Madrid
Napoli au Barcelona au Chelsea au Bayern Munich
Atalanta v Paris St Germain

### WAFUNGAJI

Hadi sasa katika michuano hiyo, straika wa Bayern Munich, Robert Lewandowski ndiye kinara wa kuzifumania nyavu, kwani ana jumla ya mabao 11 kibindoni.

| | | |
|---|---|---|
| 1. R. Lewandowski | B. Munchen | 11 |
| 2. Erling Haaland | B. Dortmund | 10 |
| 3. Harry Kane | Tottenham | 6 |
| 4. Serge Gnabry | Bayern Munchen | 6 |
| 5. Dries Mertens | Napoli | 6 |
| 6. Memphis Depay | Lyon | 5 |

## Nukuu

"Nafikiri kila mtu kwenye soka anavutiwa na Carlo (Ancelotti) kama kocha, kama humjui yeye kama mtu, basi mfahamu kama kocha. Nampenda yeye kama mtu na naweza kusema hivyo kwa kujisifu kabisa, yeye ni mmoja wa makocha bora duniani. Nafikiri ni heshima Ligi Kuu England kuwa na mtu kama Carlo. Pia ni fahari kwa Everton kuwa na kocha kama yeye," **alisema Jose Mourinho kuhusiana na mkongwe huyo.**



"Najua kuna uvumi. Sio kweli, hizo ni taarifa za kizushi. Quique Setien anaaminiwa na kila mtu, wachezaji, bodi na anafanya kazi nzuri," **Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu alisema hayo kuhusiana na tetesi za kibarua cha kocha huyo kukalia kuti kavu.**



"De Gea (David) ni mtu wa aina yake kwa upande wetu, hakuna shaka kuhusu hilo, amepitia kwenye wakati mgumu katika histori ya Manchester United. Amekuwa akipanda na kushuka, hilo ni jambo la kawaida, yeye ndio mchezaji wetu bora," **Peter Schmeichel, golokipa wa zamani wa timu hiyo aliiambia MUTV.**





# MAGOLI 10 MAKALI YA 'USIKU' LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na ongezeko la magoli yanayofungwa dakika za nyongeza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa siku za hivi karibuni kuelekea kumalizika kwa msimu wa 2019/20.

**Magoli hayo yamekuwa yakifungwa katika dakika ambazo tayari baadhi ya mashabiki wa soka wameshatoka nje ya uwanja, na wengine wameshapanda kwenye usafiri wao binafsi au ule umma.**

Magoli haya yanatokana na sababu nyingi za waamuzi kuongeza dakika za nyongeza, ikiwamo wachezaji kuchelewesha muda na hasa makipa.

Ni magoli ambayo yameongeza utamu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo tayari Simba imeshatwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, huku baadhi ya timu zikishindana kukimbia kwenye nafasi nne za chini za kushuka daraja, na zingne mbili za juu yake ambazo timu zitakwenda kucheza mechi za mtoano.

Kutokana na kuwapo magoli yanayofungwa dakika za nyongeza kwa siku za karibuni, mwandishi wa makala haya amekukusanyia jumla ya magoli 10 yaliyofungwa kwenye dakika za majeruhi na wafungaji wake.

**1. PETER MAPUNDA (MBEYA CITY VS MBAO) DK 90+3**

Mbeya City ikiwa ugenini, iliichapa Mbao FC mabao 2-1, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza, mechi iliyochezwa Oktoba 28, mwaka jana. Wakati zilipofika dakika 90 timu hizo zilikuwa sare ya bao 1-1, lakini dakika tatu za nyongeza zilitoa matokeo tofauti kabisa. Mbeya City ilipata penalti na mchezaji Peter Mapunda akauweka wavuni na Mbeya City ikapata ushindi kwenye mechi hiyo.

**2. PAUL BUKABA (NAMUNGO VS COASTAL) DK 90+4**

Hili lilikuwa ni bao la kujifunga. Ilikuwa ni dakika ya nne ya nyongeza, beki wa Namungo, Paul Bukaba alipojifunga mwenyewe na kuwapa wapinzani wao, Coastal Union ushindi wa mabao 3-1 Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, Novemba 22 mwaka jana.

Wakati wachezaji wa Namungo wakitafuta bao la kusawazisha dakika za majeruhi angalau iwe 2-2, Bukaba akajifunga mwenyewe na mechi ikaisha hivyo.

**3. HARUNA CHANONGO (MTIBWA VS KAGERA SUGAR) DK 90+3**

Novemba 26, mwaka jana, Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, ilizikutanisha timu ndugu, Kagera Sugar iliwapokea Mtibwa Sugar. Wakati Kagera Sugar ikiwa nyuma kwa mabao 2-1, ikitafuta bao japo la kusawazisha mechi iishe kwa mabao 2-2, wakajikuta wakipachikwa bao la tatu, dakika ya tatu za nyongeza, likifungwa na Haruna Chanongo na mechi ikaisha kwa Mtibwa kushinda ugenini magoli 3-1.

**4. ABDUL HILLARY (KMC VS YANGA) 90+3**

Mashabiki wa Yanga walijua kabisa timu yao ingeibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya timu ngumu ya KMC.

Dakika tatu za majeruhi zilitoka kabisa kubadilisha matokeo na kuwa sare ya bao 1-1. Ni kwamba Kelvin Yondani alimdondosha mchezaji mmoja wa KMC ndani ya eneo la hatari na KMC ikazawadiwa penalti, ambayo iliwekwa wavuni na Abdul Hillary, ngoma ikaenda sare, mechi ikichezwa Desemba 2, mwaka jana.

**5. GERSON FRAGA (SIMBA VS KMC) DK 90+3**

Mbrazil wa Simba Gerson Fraga naye yumo kwenye orodha ya wachezaji waliofunga magoli kwenye dakika za majeruhi. Yeye alifunga bao Desemba 28, mwaka jana, Simba ikiifunga KMC mabao 2-0.

Wakati Simba ikiwa inaongoza bao 1-0, huku baadhi ya mashabiki bado wakiwa hawaamini kama timu yao ingetoka uwanjani na ushindi huo, Fraga aliongeza bao la pili dakika ya tatu ya nyongeza na ubao ukasomeka 2-0.

**6. DAUDI MBWENI (SINGIDA UNITED VS MBAO) DK 90+4**

Daudi Mbweni ni mchezaji wa Singida United ambayo kwa sasa imeshashuka daraja, inachofanya ni kumalizia mechi zao tu zilizobaki. Yeye aliweka rekodi ya kufunga bao kwenye dakika ya nne ya nyongeza, siku timu yake ilipobugizwa mabao 3-1 nyumbani dhidi ya Mbao. Hiyo ilikuwa ni Februari 18, mwaka huu.

**7. AYOUB LYANGA (COASTAL VS LIPULI) DK 90+4**

Ni mechi iliyochezwa Machi 10, mwaka huu Uwanja wa Mkwakwani jijini, Tanga ikishuhudia mchezaji wa Coastal Union, Hance Rashid akifunga bao kwenye dakika ya nne ya nyongeza, Coastal ikiichapa Lipuli mabao 2-0. Wakati wachezaji wa Lipuli wakihangaika kutaka kusawazisha bao dakika hizo, Hance akaandika bao lililomaliza mchezo.

**8. PATSONS SHIGALA (MBEYA CITY VS JKT) DK 90+2**

Mbeya City ilipata ushindi wa mabao 2-0 Juni 27 mwaka huu dhidi ya JKT Tanzania Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya. Bao la pili la washindi lilipatikana dakika ya pili ya nyongeza, likifungwa na Patson Shigala.

**9. DAVID MOLINGA (YANGA VS NAMUNGO) DK 90+7**

Straika wa Yanga, David Molinga aliiokoa Yanga isipoteze mechi dhidi ya Namungo Juni 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam. Wakati kila mmoja akijua Yanga imelala kwa mabao 2-1, Molinga alisawazisha bao kwenye dakika ya saba ya nyongeza na mechi hiyo ikaisha kwa mabao 2-2.

**10. CLEOPHACE MKANDALA (PRISONS VS COASTAL) 90+8**

Wakati ikidhaniwa kuwa bao la Molinga ndiyo litakuwa limeweka rekodi ya kufungwa kwenye dakika nyingi zaidi za nyongeza, ukweli siyo hivyo.

Goli lililochelewa zaidi kwenye Ligi Kuu lilifungwa Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, likifungwa na mchezaji wa Prisons, Cleophace Mkandala.

Ilikuwa ni mechi kati ya Prisons dhidi ya Coastal Union iliyochezwa Julai 9, mwaka huu, wageni wakishinda kwa mabao 2-1.

Mkandala alifunga bao la kufutia machozi kwenye dakika ya nane ya nyongeza kwa penalti huku timu yake ikipoteza mechi hiyo.

DAVID MOLINGA

**JE, WAJUA?**



Pep Guardiola ambaye kwa asili alikuwa kiungo mkabaji, alichezeshwa zaidi nafasi ya kiungo mchezeshaji na alikuwa kwenye kikosi cha Barcelona pamoja na Johan Cruyff kushinda taji la kwanza na Kombe la Ulaya kwa klabu hiyo mwaka 1992. Pia alikuwa nahodha wa Hispania kati ya mwaka 1997 na 2001.



# Mpango wa uendelezaji viwanda vidogo, kati rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amezindua mpango wa uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati ili kuwawezesha kiuchumi wajasiriamali wadogo na wa kati.

Hatua hiyo inalenga kutatua tatizo la upatikanaji wa ujuzi, masoko na mitaji.

Akizindua mpango huo, Waziri Mhagama alisema utasaidia kuongeza kasi ya ujenzi na ukuaji wa uchumi kwa kutengeneza mazingira wezeshi na kuandaa mazingira yenye mfumo wa kibiashara itakayorahisisha kutengeneza uzalishaji wenye tija.

Alisema mpango umejikita katika kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanasaidiwa kuongeza ujuzi na kuhimili ushindani katika masoko ya ndani na nje. "Pia kuwezesha viwanda kupata vifaa vya kisasa kama mitambo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji ili uwe na tija, kutoa mikopo yenye riba nafuu ili kupanua shughuli za uzalishaji pamoja na kuongeza kinga za hifadhi za jamii kwa wajasiriamali," alisema.

Aidha, alisema kwa kupitia mpango huo wenye viwanda na wajasiriamali wamepewa fursa ya kupata mitaji, hivyo kutengeneza fursa za ajira kwa vijana wengi wanaohitimu vyuo katika ngazi mbalimbali. Alifafanua sekta ya viwanda imeendelea kuwa na tija katika kuchangia ongezeko la pato la Taifa kwa kuongezeka kwa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

"Sekta ya viwanda katika pato la Taifa kwa mwaka 2019 ilikuwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 8.05 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 0.45 na hii ni matokeo ya kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani katika kipindi hicho," alisema.

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema mpango huo umesadifu mikakati ya nchi katika uendelezaji viwanda na imekuja wakati mwafaka.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, alisema mpango umeainisha namna bora ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwamo la kukuza mitaji na kuimarisha vyanzo vyao vya mapato na kukuza akiba na mikopo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii(NSSF), William Erio, alisema mfuko huo umetoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya utoaji mikopo kwa wajasiriamali hao wenye viwanda wanaojishughulisha katika kuzalisha bidhaa ili kuongeza mnyororo wa thamani.

"Tupo taasisi nne ambapo NEEC ndio msimamizi wetu, pia kuna SIDO na VETA ambazo zinahusika na utambuzi wa miradi na utoaji wa mafunzo, sisi tumeshatoa Sh. bilioni tano ambazo zipo kwenye Benki ya Azania na zitaendelea kutolewa kulingana na uhitaji," alisema.

Alitoa wito kwa wajasiriamali kuchangamkia fursa hiyo kwa kuandaa maandiko ya kuomba fedha hizo huku akiwataka kuzitumia kwa malengo watakayoainisha kwenye maombi yao na si vinginevyo.



Wakulima wa mtama wakiwa katika uvunaji wa mbegu bora ya zao hilo, aina ya masia katika shamba la Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Kata ya Hombolo jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sheikh ataja wa kuchaguliwa Oktoba

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewataka Watanzania katika uchaguzi utakaofanyika Oktoba mwaka huu wahakikishe wanachagua viongozi bora na wenye hofu ya Mungu.

Wito huo aliutoa Jumamosi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu rai yake kwa jamii katika kuelekea uchaguzi mkuu.

Alisema Taifa linategemea kupitia uchaguzi huo kupata viongozi wenye ari ya kuleta maendeleo kwa ajili ya Watanzania. "Ni matamanio yetu Watanzania wapate viongozi wa jinsi hii na si vinginevyo," alisema.

Aliwataka Watanzania kutofanya makosa yatakayo gharimu kwa miaka mitano ijayo kwa kuwachagua viongozi wanaotoa rushwa. "Watanzania mjihadhari na viongozi wanaotaka uongozi kwa kuwanunua kutokana na uwezo wao wa kifedha," alisema. Aliwahimiza kuwa makini na viongozi wanaowania ubunge na udiwani ambao hawana sera zaidi ya kutaka nafasi hizo.

"Miaka mitano inaweza kuwa ya utumwa ikiwa tu, Watanzania watafanya makosa kwa kuchagua viongozi watoa rushwa na wapenda madaraka," alisema.

Alisisitiza wapate viongozi ambao ni chaguo la Mungu na watakaoshirikiana na viongozi wa dini katika kufanya kazi.

"Kama anavyotuhimiza Rais wetu katika kumtanguliza Mungu kwa kila jambo, hata Watanzania kwenye uchaguzi huu waombe wapate viongozi watakaokuwa na maadili ya kiroho," alisema.

# Fedha zatengwa fidia barabara za mzunguko Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema imeshatenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wanaopitiwa na mradi wa barabara za mzunguko katika Jiji la Dodoma.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, katika hafla ya utiaji saini ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami, zenye urefu wa kilomita 112.3 na zitagharimu Sh. bilioni 494, ikiwa ni mkopo wenye riba nafuu, kutoka Benki ya Maendeleo Afrika.

Alisema fidia hiyo itatolewa kwa mujibu wa sheria kwa kufuata utaratibu na siyo vikundi vya mitaani.

"Watu wamekuwa wakinifuata ofisini kwangu na kujitambulisha wao ndiyo wawakilishi wa kamati za ufuatiliaji fidia, nimewafukuza kwani mkuu wa wilaya hayupo mimi nitazunguzaje na wewe kuhusu fidia hata zimekuja" alisema Kamwelwe.

Alibainisha mradi huo utajengwa na makandarasi wawili ambao ni CCECC pamoja na AVIC International Kampuni zote kutoka China.

Alisema, ujenzi wa mradi huo, utakuwa ni sehemu ya mtandao wa barabara za jiji hilo, ambao utasaidia kuunganisha mikoa pamoja na nchi za jirani.

"Ujenzi wa mradi huu kwanza utatoa fursa ya ajira kwa wananchi, lakini wito wangu ni kuhahakikisha kuwa makandarasi wanamaliza kazi yao katika muda uliwekwa kwa mujibu wa mkataba," alisema Kamwelwe.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale, akitoa maelezo kuhusu mradi huo alisema kuwa fedha za utekelezaji wa mradi huo ni kutoka Benki ya Maendeleo Afrika na kiasi kingine ni kutoka serikalini.

"Fedha ya ujenzi wa mradi huu ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kiasi cha Sh. bilioni 412, na serikali itachangia kiasi cha Sh. bilioni 82, sawa na asilimia 16.5 ya kiasi chote cha fedha," alisema Mfugale.

Alifafanua kuwa, awamu ya kwanza ya mradi huo itajengwa na mkandarasi CCECC, ambapo atajenga barabara yenye urefu kwa kilimita 52.3 kwa gharama ya Sh. bilioni 100.84.

Alisema awamu ya pili, itajengwa na mkandarasi AVIC International, ambapo atajenga barabara yenye urefu wa kilomita 60, kwa gharama ya Sh. bilioni 120.86 bila kodi ya ongezeko la thamani.

"Kipande cha kwanza cha urefu wa kilomita 52.3, mkandarasi atajenga kwa muda wa miezi 39, na kile cha pili chenye urefu wa kilomita 60, kitajengwa kwa muda wa miezi 42," alibainisha Mfugale.

Alifafanua kuwa, pia kutakuwa na miradi mdogo itakayotekelezwa katika vijiji ambavyo barabara hiyo itapita. Alisema, miradi hiyo midogo ni pamoja na ujenzi wa zahanati na magari matano ya kubeba wagonjwa, ujenzi wa shule, uchimbaji wa visima vya maji pamoja na ukarabati wa barabara katika maeneo ya mradi wa barabara ya mzunguko, ambapo utagharimu Sh. bilioni 16.272.

"Hadi sasa toka nimeingia TANROADS Benki ya Maendeleo Afrika, wameweza kujenga barabara kilomita 1,704 na wametoa mkopo kiasi cha Sh.trilioni 3.169," alisema.

"Na katika mwaka 2018/19 walitoa mkopo wa Sh. bilioni 800.9 na serikali yetu ilitoa Sh. bilioni 137.5 kwa ajili ya miradi mbalimbali, ikiwamo ujenzi wa Uwanja wa Ndege Msalato Dodoma na daraja la Pangani," alieleza Mfugale.





# Njeza ajivunia huduma za jamii Mbeya Vijijini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa zamani wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza (CCM), amesema uboreshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja unaoendelea katika jimbo hilo, utasaidia kuboresha huduma za kijamii ikiwamo usafiri na usafirishaji.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 mpaka Bunge lilipovunjwa mwezi uliopita.

Alisema kwa sasa barabara nyingi ambazo zilikuwa ni kero kwa wananchi zimeanza kuboreshwa ikiwamo barabara ya Inyala- Simambwe yenye urefu wa Kilomita 16.7 ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami.

Alisema barabara hiyo inajengwa na Wakala wa Barabara za Mijini na vijijini (TARURA) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), na kwamba barabara hiyo itasaidia wakulima kusafirisha mazao yao kutoka mashambani kwenda sokoni kwa urahisi.

Alisema barabara hiyo itasaidia kupunguza umbali wa kwenda kuanzia Uyole jijini Mbeya ambapo kuna ongezeko la zaidi ya kilomita 10 kwenda kuunganisha Inyala.

"Eneo hilo ni miongoni mwa maeneo ambayo wananchi wanazalisha sana mazao lakini usafirishaji ndio ilikuwa tatizo, sasa kipande hiki kikikamilika kitakuwa kimewafungulia mlango mpya wa kiuchumi wananchi hawa," alisema Njeza.

Aliyataja baadhi ya mazao yanayozalishwa kwa wingi katika eneo hilo ni viazi mviringo, mahindi, maharage, kabichi na mazao ya miti zikiwamo mbao.

Pia alisema barabara ya Mbalizi Mkwajuni kwa sasa inapitika vizuri baada ya kuanza kuboreshwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) pamoja na barabara ya Mbalizi- Isongole ambazo zote alisema zina umuhimu kwa jamii.

Alisema bara hizo zitarahisisha kuwasafiria pia wagonjwa wanaopewa rufani kwenda kwenye hospitali kubwa kutoka kwenye vituo vya afya vya Ikukwa, Santilya na Ilembo ambayo ni maeneo ya pembezoni.

"Eneo la Ukanda wa Umalila ndiko wakulima wa pareto na kahawa wapo, lakini kutokana na ubovu wa barabara bei za mazao haya ziko chini sana, sasa uboreshaji wa barabara hizi utasaidia hata bei kuendana na gharama za uzalishaji," alisema Njeza. Vilevile alisema serikali imesaidia kuboresha huduma za afya kwa kujenga vituo viwili, kukipanua kimoja na kujenga Hospitali ya Wilaya ambayo ipo Inyala.

Pia alisema jimbo lake ni miongoni mwa maeneo ambayo yamenufaika kwa kiasi kikubwa na miradi ya elimu ikiwamo ujenzi wa miundombinu na kugharimia elimu bila malipo ambayo imesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa.

# Kilimo 'chaibeba' Tanzania uchumi wa kati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kimesema sekta ya kilimo imechangia kwa kiwango kikubwa kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati unaochagizwa na maendeleo ya viwanda.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anakagua maandalizi ya vipando vya mazao mbalimbali kwa ajili ya Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayotarajiwa kufanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Alisema viwanda vingi ambavyo vimeanzisha hapa nchini vinategemea malighafi zinazotokana na mazao mbalimbali ambayo mengi yanazalishwa ndani ya nchi na hivyo akasisitiza kuwa taasisi hiyo itaendelea kutoa mafunzo kwa wananchi ili waimarishe zaidi uzalishaji.

Alisema kwa sasa taasisi hiyo imegundua teknolojia zaidi ya 40 ambazo zitasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ambao utaliwezesha taifa kujitosheleza kwa chakula, malighafi za viwandani na ziada kuuzwa nje ya nchi.

"Kutokana na umuhimu wa kilimo, tumeamua kuwasaidia wananchi kujifunza teknolojia mbalimbali za kilimo kwa mwaka mzima kuanzia Agosti mosi mwaka huu, miaka iliyopita wananchi walikuwa wanaishia kujifunza kwenye maonyesho ya Nanenane pekee," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema mbali na teknolojia walizobuni pia wamezalisha mbegu za mazao mbalimbali ambazo zitasambazwa kwa wananchi na kuelekezwa mbinu za kisasa za uzalishaji.

Dk. Bucheyeki alisema taasisi hiyo inawakaribisha wananchi wa maeneo mbalimbali kwenda kujifunza teknolojia za kilimo kwenye taasisi hiyo wakati wowote hata kama sio msimu wa kilimo.

Pia alisema taasisi hiyo ina maabara ya kisasa ya kupima virutubisho mbalimbali vilivyomo kwenye udongo ili kuwashauri wananchi kulima mazao kulingana na aina ya udongo wa kwenye mashamba yao.

Baadhi ya wananchi walitembelea mashamba ya taasisi hiyo kwa ajili ya kujifunza, walisema mafunzo wanayoyapata yamewasaidia kuondokana na kilimo cha mazoea ambacho kilikuwa ni kwa ajili ya kujikimu kwa chakula na sasa wanazalisha kibiashara.

Zawadi Mzumbwe kutoka Kata ya Isuto Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema awali kabla hawajaenda kujifunza kwenye taasisi hiyo, walikuwa wanatumia mbegu za asili ambazo tija yake ilikuwa ndogo.

Alisema walikuwa wanapata kuanzia gunia tatu mpaka saba za mahindi kwenye ekari moja lakini baada ya kupata mafunzo ya matumizi ya mbegu za kisasa na mbinu za kilimo bora wanapata kuanzia gunia 15 na kuendelea.

"Tulikuja kama kikundi tukajifunza kilimo cha kisasa, walituuzia mbegu bora ambazo baada ya kuanza kuzitumia tulibaini kuwa zina tija kubwa maana wao wanasema unaweza ukavuna mpaka gunia 35, sasa hivi tumekuja kujifunza kilimo cha viazi mviringo," alisema Mzumbwe.

Mzumbwe aliwashauri wananchi wa maeneo mengine ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenda kupata mafunzo kwenye taasisi hiyo ili kuboresha kilimo.



Mwonekano wa eneo la Barabara ya Inyala- Simambwe katika Kijiji cha Inyala Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya baada ya nyumba za wananchi zilizokuwa zimejengwa kwenye hifadhi ya barabara hiyo kubomolewa kupisha upanuzi wake. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanahabari wapongezwa elimu ya corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imevipongeza vyombo vya habari mbalimbali mkoani hapa kwa kusaidia kuelimisha wananchi kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo kuwaongezea uelewa wa kujikinga na ugonjwa wa corona ambao umekuwa tishio duniani.

Ofisa Afya wa Mkoa huo wa Mbeya, Mashaka Juma, alisema vyombo vya habari vimesaidia kusambaza elimu ya kujikinga na ugonjwa huo kuanzia mara ya kwanza ulipotangazwa kuwa umeingia nchini mpaka sasa.

Alisema pamoja na kwamba kwa sasa ugonjwa huo umepungua duniani, lakini bado wananchi wanatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari za kuepuka ugonjwa huo, hivyo akaviomba vyombo vya habari kuendelea kusambaza elimu.

Mashaka alisema Tanzania ni miongoni mwa mataifa duniani ambayo yamefanikiwa kwenye mapambano ya ugonjwa huo, ambapo alisema wananchi walikuwa wanatumia mbinu mbalimbali za kuukabili huku wakiendelea na shughuli za maendeleo.

"Rais wetu alipotangaza wananchi kuacha kutishika na ugonjwa huu na kuendelea kuchapa kazi, wengi walihamasika na kuendelea na kazi zao mpaka sasa, serikali haikufunga mipaka kama ilivyokuwa kwenye mataifa mengine, vyombo vya habari mlitusaidia sana kutangaza habari hizi na mimi naamini nanyi ni sehemu ya ushindi," alisema Mashaka.

Alisema pamoja na kwamba ugonjwa huo umepungua, lakini wananchi bado wanahamasishwa kuendelea kuchukua tahadhari kwa maelezo kuwa Tanzania sio kisiwa na badala yake bado kuna mwingiliano wa wananchi kutoka katika mataifa mbalimbali duniani.

Alisema baadhi ya mataifa hayo bado ugonjwa huo ni tatizo, hivyo kuna uezekano wengine wakasafiri kutoka kwenye mataifa yao kuja Tanzania wakiwa wana maambukizi na wakawaambukiza wanaochangamana nao.



# Ndege za kimataifa zaanza kutua Z'bar kwa kishindo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATALII na abiria kutoka mataifa mbalimbali ni miongoni mwa wasafiri 80 waliotua juzi katika kiwanja cha kimataifa cha Abeid Amani Karume Zanzibar (AAKIA).

Abiria 80 hao waliingia Zanzibar na Shirika la Ndege la Qatar Air na ndege ya Dreamliner A 787, wakiingia visiwani humo baada ya kupungua kwa ugonjwa wa COVID-19 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufungua rasmi safari za anga.

Abiria hao walitua saa 2:30 juzi wakifuata taratibu zote za tahadhari za kiafya zilizowekwa uwanjani humo.

Akizungumza na wanahabari, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Mulhati Yussuf Said, alisema, kiwanja kimeanza kupokea ndege kutoka mashirika mbalimbali.

Alisema shirika hilo lilisitisha safiri za anga tangu Aprili 9 mwaka huu baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa COVID -19 ulioyakumba mataifa mbalimbali na baadhi ya safari za anga zimeanza rasmi.

Said alisema kuwasili kwake ndege hiyo, kumeonyesha dalili nzuri kuwa sasa ugonjwa huo unaendelea kupungua na kumekuwapo kwa hali ya kuridhika kiafya juu ya janga la corona.

Alisema mashirika mengi yanaendelea kufanya mawasiliano na kiwanja hicho ili kuanzisha safari za anga na safari.

Hivyo, aliwataka Watanzania walioko nje na ndani ya nchi kueneza ujumbe kuwa kiwanja cha AAKIA kipo salama na wanaendelea kupokea abiria bila ya wasiwasi.

Ofisa Uhamiaji Mfawidhi katika kituo cha uhamiaji wa AAKIA, Bakari Mohamed Ameir, alisema wamekuwa na utaratibu bora kwa wageni wanaoingia katika kiwanja hicho huku wakizingatia usalama zaidi kujiepusha na maradhi.

Ameir aliwataka wageni kuendelea kutembelea mtandao wa Uhamiaji kwa ajili ya kuangalia utaratibu wa kuomba kibali cha kuingia nchini na kuondokana na usumbufu.



Amos Malima, Mkazi wa Kijiji cha Vilabwa wilayani Kisarawe mkoani Pwani, akijaza mafuta ya petroli kwa ajili ya kuyauza rejareja kwa waendesha pikipiki maarufu 'Bodaboda' katika mazingira yasiyo salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka mabadiliko uongozi wa shehia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Unguja Rajab Ali Rajab, amewataka masheha kupitia upya kamati walizozianzisha ili kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa wajumbe wake.

Alisema kuna baadhi ya shehia kumekuwapo na tatizo la ushiriki mdogo wa wanakamati zinapotokea ziara ama shughuli za kijamii hali ambayo inaleta usumbufu kwa serikali inapofanya ufatiliaji wa huduma za kijamii

Akizungumza jana katika kikao cha pamoja na masheha hao ofisini kwake Mahonda, Rajab alisema lengo la kuundwa kwa kamati mbalimbali katika shehia ni kuwarahisishia wananchi kupata huduma muhimu kwa wakati sahihi pamoja na kuusaidia uongozi wa shehiya katika majukumu yake ya kila siku

Aliwataka masheha hao kusimamia utaratibu uliowekwa na serikali kwa kuhakikisha rasilimali hasa ardhi na na maeneo ya mabondeni hayavamiwi na wananchi na kutumiwa kinyume na utaratibu

Kwa upande wao masheha hao walisema kuna tatizo la uelewa kuhusu umuhimu wa kupata vibali vya ujenzi hali ambayo inaleta usumbufu mamlaka husika inapositisha shughuli za ujenzi kwa wananchi.

Waliiomba ofisi ya mamlaka ya maji wilayani humo kutatua tatizo la kukosekana huduma hiyo kwa wananchi ili kila mmoja aweze kulipia maji hayo bila ya vikwazo.

# Asisitiza kujali zaidi amani kuelekea uchaguzi Oktoba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MCHUNGAJI Kiongozi wa Makanisa ya Kipentekoste Zanzibar (PEFA), Daniel Kwilemba Kwiyeya, amesisitiza umuhimu wa Watanzania kulinda zaidi amani wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Aliitaka jamii kusimamia na kudumisha amani na utulivu katika kipindi hiki na pia kuchagua viongozi watakaowafaa na si wasindikizaji.

Alitoa ushauri huo jana katika hafla ya kuzinduwa jengo la kanisa hilo liliopo Kisauni, Unguja.

Alisema kuwa katika kipindi cha uchaguzi hujitokeza mambo mengi ambayo mengine husababisha kutokea kwa vurugu.

Alieleza kuwa kipindi hiki jamii inatakiwa kuwa makini na isiruhusu matakwa yao yawatawale ili kuepusha migogoro itakayopelekea kuvunjika amani.

Kuhusu kanisa, alisema mbali na kufanya ibada pia limejengwa na litakuwa likihusisha shughuli mbali mbali za kijamii na kuiomba jamii kujitokeza kulitumia.

Aidha, alisema kuwa katika eneo hilo la kanisa kuna shule ambayo inafundisha madili ya Kizanzibari.

Ujenzi wa kanisa hilo unatarajiwa kutumia milioni 100 hadi kukamilika kwake na hadi sasa zimetumia shilingi milioni 48.

# Mradi kutokomeza ukatili kuwafikia 50,000

**Na Happy Severine,** ILIMA

ASASI ya Kawiye Development Social Development yenye makao yake makuu wilayani Maswa mkoani Simiyu inatarajia kuwafikia wananchi 50,000 katika mradi wa awamu ya pili ya utekelezaji wa kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Itilima.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi wa asasi hiyo, Ezekiel Kassanga, amesema mradi huo unakusudia kusaidia na kuchangia jitihada za utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto wa mwaka 2017-2018 hadi 2018-2020.

"Katika mradi huo Asasi ya Kawiye inakusudia kujenga na kuimarisha uelewa wa jamii kuhusu kuepuka kutenda vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto ikiwapo ndoa za utotoni, vipigo vya wanawake pamoja na ukatili wa kiuchumi," alisema Kasanga.

Mkurugenzi hiyo alieleza kuwa dhamira kuu ya mradi huo ni kuwezesha jamii kuwa na uelewa wa athari za vitendo vya ukatili na uthubutu wa kuchukua hatua endelevu katika kutokomeza vitendo hivyo wilayani Itilima.

Alifafanua kuwa katika utekelezaji huo utahusisha mafunzo mbalimbali kwa njia ya warsha kwa wanajamii, kutoa machapisha, habari mbalimbali yatakayobandikwa barabarani ili kueneza ujumbe uweze kuifikia jamii kwa haraka.

Mradi huo wa awamu ya pili wa tokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wilayani Itilima mpaka kukamilika kwake utagharimu kiasi cha Sh. milioni 30,000,000 ambazo ni ruzuku iliyotolewa na Shirika lisilo la kiserikali la The Foundation for Civil Society na kutekelezwa na asasi hiyo.

# Bosi TIC atumbuliwa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amemteua Dk. Maduhu Kazi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, kabla ya uteuzi huo alikuwa meneja wa idara ya sera za kibajeti na madeni wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kiongozi huyo anachukua nafasi ya Godffrey Mwambe na uteuzi wake umeanza jana.

# Bar'wani kutetea kiti chake Lindi Mjini kupitia CHADEMA

**Na Said Hamdani,** LINDI

MBUNGE wa zamani wa Lindi Mjini, Salum Khalfani Bar'wani kwa kupitia tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), amejitosa kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika nchini mwaka huu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Katibu wa CHADEMA Jimbo la Lindi Mjini, Zingatia Mohamed, aliyaeleza hayo alipokuwa anazungumza na wanahabari.

Zingatia alisema Julai 04/2020, ofisi yao ilifungua milango kuwataka wanachama wenye nia ya kugombea kujitokeza kuchukuwa fomu za kuomba ridhaa ndani ya chama, ambapo 21 kati yao 19 wamechukua fomu za kuwania udiwani wa kata na viti maalum, huku wawili wakiwania ubunge.

Kwa upande wa ubunge, Zingatia aliwataja waliojitokeza kuchukua fomu ni Bar'wani na Hemedi Ally, Katibu wa Itikadi na Uenezi CHADEMA Taifa.

Alisema alisema, watia nia nafasi ya udiwani ni 19, wakiwamo 11 wanaowania nafasi za kata na 8 viti maalum.

Aliwataka wanachama waliojitokeza kuchukua fomu kuwania nafasi za uongozi ngazi ya majimbo na kata kujiepusha kushiriki vitendo vya rushwa, badala yake wafuate taratibu za chama chao.

Mtia nia nafasi ya ubunge wa Jimbo la Lindi Mjini, Hemedi Ally, alisema kilichomfanya awanie nafasi hiyo ni kutaka kurejesha heshima ya jimbo hilo kwa wananchi.

Aisema Jimbo la Lindi kabla na baada ya Uhuru lilikuwa na viwanda vilivyosaidia wananchi kupata ajira mbalimbali zilizowawezesha kuendesha maisha yao ya kila uchwao tafauti na ilivyo hivi sasa.



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk.Severine Lalika, akimkabidhi mmoja wa wanachama wa Chama cha Madereva na Makondakta Mkoa wa Mwanza kadi ya bima ya afya ya CHF iliyoboreshwa. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# NBC yafuzu kuwania tuzo za ubora Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC Tanzania imeteuliwa kuwania tuzo za ubora za Afrika katika kuwahudumia wajasiriamali ambazo zinaakisi ufanisi wa huduma za kibenki na kifedha katika bara la Afrika.

Katika tuzo hizo ambazo zinashindaniwa na benki zaidi 200, benki ya NBC imefanikiwa kuingia kwenye orodha ya benki tano bora zinazowania tuzo ya Benki Bora ya mwaka ya wajasiriamali (SME Bank of the year) hatua muhimu zaidi kufikiwa na benki ya Kitanzania ndani ya mwaka huu.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara cha Benki hiyo, Elvis Ndunguru, alisema inakuwa ni benki pekee nchini kuchaguliwa kuwania tuzo hiyo inayowaniwa na benki nyingine barani Afrika ikiwamo Benki ya Industry na Benki ya Sterling zote kutoka Nigeria, Benki ya Misr (Misri) pamoja na Ecobank.

Alisema kundi hilo linalenga kuthibitisha ubora wa taasisi za kifedha katika kusaidia na kubadilisha maisha ya wajasiriamali katika bara la Afrika.

"Tunafurahi sana kufikia hatua hii ya kuwania tuzo hizi bora barani Afrika. Tunataka kuongeza shukrani zetu kwa wateja na wadau kwa imani yao endelevu, ushirikiano, maoni na kuhusika katika kuboresha huduma zetu kwa wajasiriamali," alisema Ndunguru.

Alisema benki hiyo imejipambanua kama kituo kimoja chenye mahitaji yote ya wajasiriamali kwa kutoa huduma mahususi na maalum zinazoakisi mazingira ya biashara ya ndani kwa lengo la kukuza na kuendeleza sekta ya wajasiriamali nchini.

"Katika kuhakikisha hilo, benki imeendeleza klabu ya biashara (NBC-Club) ambayo inawaunganisha wajasiriamali na kuwawezesha kufanya safari za kibiashara, huduma za bure za ushauri wa kibiashara na uendeleo maalum katika baadhi ya huduma, hatua ambayo inalenga kuleta mabadiliko katika sekta hii muhimu," alisema Ndunguru.

Utafiti unaonyesha kuwa, sekta ya wajasiriamali inachangia asilimia 35 ya Pato la Taifa (GDP), huku ikiajiri zaidi ya watu milioni 5.2 nchini.

Hata hivyo alisema sekta hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo ufikiwaji mdogo wa huduma za kifedha, sababu iliyotajwa kuwa ndio iliyopelekea benki ya NBC kuwekeza zaidi katika kuboresha mazingira ya biashara kwa kutoa huduma bora na kwa gharama nafuu.

Sherehe ya tuzo hizo inatarajiwa kufanyika Agosti 26 mwaka huu wakati wa Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Afrika chini ya usimamizi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Tuzo hizo huleta pamoja viongozi wa sekta ya kibenki kutoka Afrika na ulimwenguni kusherehekea mafanikio ya vinara wanaongoza ukuaji na maendeleo na kubuni fursa mpya za kiuchumi kwa raia na jamii kote barani na kuhamasisha vizazi vipya vya wadau wa sekta ya benki wanaojenga mustakabali wa Afrika.

HABARI KITAIFA

# Sababu kusitishwa uagizaji mtama nje

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imedhamiria kukomesha uagizaji wa zao la mtama kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya viwanda nchini baada ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ilonga iliyopo wilayani Kilosa mkoani Morogoro kugundua na kuzalisha aina saba za mbegu za zao hilo na uwele.

Mbegu hizo zitatumika kama malighafi kwenye viwanda ili kutengeneza vinywaji laini na vikali hapa nchini.

Tayari TARI Ilonga imeanza mchakato wa kuwashirikisha wakulima katika vijiji vya Ulaya Mbuyuni, Kibaoni, Mhenda na Ngole vilivyopo Wilaya ya Kilosa kwa kuwaonyesha mbegu hizo zilizopandwa katika shamba darasa lililopo katika kijiji cha Kibaoni ili waweze kuchagua aina za mbegu zilizo bora ili ziweze kupasishwa kwa ajili ya kilimo hicho baada ya kufanyika kwa majaribio katika kituo cha utafiti.

Akizungumza katika maonyesho ya mbegu hizo mtama na uwele, Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk. Joel Meliyo, alisema pamoja na kusaidia serikali kutumia fedha nyingi kwa kuagiza ya mtama kutoka nje ya nchi, lakini wanataka kusaidia wakulima kupata chakula cha kutosha pamoja na ziada kwa ajili ya kuviuzia viwanda vya nchini.

Alisema asilimia 60 ya mtama unautumika kwenye viwanda nchini umekuwa ukiagizwa kutoka nje ya nchi wakati uwezo wa kuzalishaji hapa nchini upo hivyo wao kama watafiti wameamua sasa kuja na mbegu hizo za teknolojia ya kisasa zilizotokana na mbegu za hapa nchini ili kuwasaidia wakulima kulima kilimo hicho kwa manufaa ya viwanda.

Naye Mratibu wa Utafiti na mgunduzi wa zao la mtama nchini kutoka TARI Ilonga, Dk. Justin Ringo, alisema baada ya ugunduzi wa mbegu hizo wameamua kuzipeleka kwa wakulima ili kuzitambua mbegu hizo na kuzipeleka katika hatua inayofuata kwa lengo la kuzianishwa kwa matumizi ya wakulima.

Dk. Ringo alisema kupitia mradi wa mtama unafahamika kama avisa, wanatarajia zitapatikana mbegu aina nne za mtama na nne za uwele kupelekwa hatua inayofuata na kwamba mbegu hizo ni tofauti na zile anazotumia wakulima kwa kuwa zina uwezo wa kutoa wastani wa tani nne mpaka tano kwa hekta za chakula kwa miezi miwili ukilinganisha na za wakulima zinatoa chakula ndani ya miezi minne mpaka mitano chini ya tani moja kwa hekta.

Mtafiti na mgunduzi wa mbegu za mtama, uwele na ulezi, Emanuel Mwenda, akizungumzia kuhusu hali ya soko la mtama na uwele nchini, aliwaondoa hofu wakulima hao na kutaka walime kwa wingi kilimo cha mtama mweupe kwa kuwa makumpuni ya bia Tanzania yanatumia mtama huo na uwele kwa ajili ya uzalishaji wa vinywaji hivyo na kwamba kuna mahitaji makubwa kwajili ya uzalishaji huo.

Mmoja wa wakulima wa kijiji cha Mhenda, Tatu Magongo, alipongea watafiti hao kwa kuwaletea mbegu za mtama za muda mfupi wa miezi miwili zenye tija kubwa ukilinganisha na zile wanazotumia za miezi mitano na kuahidi kuanza kilimo hicho mara tu mbegu hizo zitakapopitishwa kwa kuwa zitawaletea ukombozi na kuondokana na umaskini.

Naye Mratibu wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Mahusiano wa TARI Ilonga, Magreth Mchomvu, alisema baada ya mbegu hizo kupitishwa atahakikisha teknolojia hizo zinawafikia wakulima kwa wakati na katika maeneo yanayozalisha mtama kwa wingi ili waweze kulima kilimo cha kisasa chenye tija na kupata mavuno mengi.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema TARI kwa kutumia watafiti wake kutoka katika vituo 17 wamejipanga kuhakikisha wanabuni tafiti zitakazosaidia uzalishaji wa malighafi ili kuunga mkono jitihada za serikali kuelekea uchumi wa viwanda.

## TAKUKURU yawapa angalizo wagombea ubunge na udiwani

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi, imetoa onyo kwa wananchi wanaohitaji kuwania nafasi za ubunge na udiwani, katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika nchini mwaka huu, kujiepusha na vitendo vya utoaji rushwa.

Wameonywa kuwapa rushwa wajumbe ili wawapitishe wakati wa kura za maoni.

Mkuu wa taasisi hiyo mkoani humo, Stephen Chami, alitoa angalizo hilo mjini Lindi, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusiana na utendaji wa taasisi hiyo.

Alitoa onyo hilo kufuatia baadhi ya watia nia wa nafasi ya ubunge kuanza kutumia fedha kwa ajili ya kushawishi wajumbe kupitisha majina yao wakati wa vikao vya kura za maoni.

Hivi karibuni mmoja wa watia nia kwa nafasi ya ubunge Jimbo la Mtama, mkoani Lindi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Nahuka Huka alikamatwa akiwa na wajumbe akituhumiwa kugawa fedha kwa wajumbe ili wampitishe kwenye kura za maoni.

Alisema ni wajibu kwa watia nia wakazingatia sheria, kanuni na taratibu ili kujiepusha na vitendo vya utoaji rushwa wakati wa kura za maoni kwa ajili ya kupitisha majina yao kinyume cha hapo hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mkuu huyo wa TAKUKURU mkoani Lindi, alisema katika kipindi hiki cha uchaguzi, taasisi hiyo imejipanga vizuri kuhakikisha vitendo vya rushwa havipewi nafasi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu na utakaofuata.



Mratibu wa utafiti na mgunduzi wa zao la mtama hapa nchini kutoka TARI Ilonga, Dk. Justin Ringo (kulia), akitoa maelezo kwa wakulima wa vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Kilosa kuhusu mbegu mpya ya mtama inavyoweza kuzaa kwa kipindi cha muda mfupi ukilinganisha na mbegu za kienyeji wanazotumia wakulima katika wilaya hiyo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Vyombo vya habari vyakumbushwa utoaji wa elimu juu ya ukatili kijinsia

**Na Elizabeth Zaya**

VYOMBO vya habari vimetakiwa kuibua na kufuatilia kwa undani habari zinazoleta suluhisho juu ya vitendo vya ukatili vinavyotokea katika jamii.

Mkurugenzi wa Shirika la Mabadiliko na Kujenga Ushirikiano kwa Wote(TIBA), Malcela Lungu, akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, alisema bado kuna vitendo vya ukatili vinavyoendelea ndani ya jamii lakini vingi vimekuwa haviripotiwi.

Alisema matukio mengine ya ukatili yamekuwa hayaripotiwi kutokana na kukosekana kwa elimu ya kutosha kwa jamii juu ya athari zake na namna ya kuviripoti katika vyombo vya dola.

"Vyombo vya habari kama daraja muhimu, kuna haja ya kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuisaidia athari zake na namna wanavyoweza kuviripiti katika vyombo vya dola," alisema Lungu.

Pia alitoa wito kwa makundi mbalimbali katika jamii kujenga tabia ya kutokuvifumbia macho vitendo hivyo.

"Kuna makundi mbalimbali katika jamii, kuhakikisha kwamba nao wanawajibika kukemea vitendo hivyo vya ukatili, hakuna kuliachia kundi moja tu," alisema Lungu.

Pia alisema kuna umuhimu kwa wanaume kushiriki katika kupambana na kupinga vitendo hivyo vya ukatili badala ya kuwaachia wanawake pekee ikiwamo kuanzisha majadiliano hayo katika vijiwe mbalimbali.

"Kuna haja ya kurudisha tena vile vijiwe vya kahawa ambavyo hutumika kujadili mambo mbalimbali, ili tuanze kujadili kwa kina namna ya ushiriki wa wanaume katika mapambano ya ukatili huo," alisema Lungu.

"Kuna matukio mengi ambayo yanaendelea kuripotiwa kuhusu wanaume kuwanyanyasa wanawake ikiwamo kuwapiga, ubakaji, kuna masuala ya mimba za utotoni bado zinaripotiwa, hizi zote zinahitaji pia ushiriki wa wanaume kwa sababu bado kuna gepu kubwa la ushiriki wa kundi hili."

Alisema ili kufanikiwa kupambana na suala la ukatili lazima makundi yote katika jamii yashiriki.

"Tunataka pia wanaume wawe machampioni katika hili, wasijiweke nyuma kwa sababu na wao hili jambo linawahusu, tukishiriki kwa pamoja tutashinda," alisisitiza Lungu.

Malcela alivikumbusha pia vyombo vya habari kuendelea kutoa elimu namna ya jamii kuendelea kuchukua tahadhari kuhusu ugonjwa wa corona.

"Tunashukuru Mungu ametusaidia kwa kiwango kikubwa kuhusu janga hili, lakini tusibweteke na hii hali, tuendelee kuchukua tahadhari, ninaomba vyombo vya habari visichoke, viendelee kutoa elimu," alisema.

# GUARDIOLA ASIFIA KIWANGO CHA STERLING




**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesifia maendeleo ya Raheem Sterling baada ya mshambuliaji huyo kufunga 'hat-trick' wakati Manchester City wakiibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Brighton and Hove Albion.

Sterling sasa amefikisha mabao 27 msimu huu, yakiwa ni mengi zaidi aliyofunga kwa msimu mmoja.

Guardiola alimsifia mchezaji huyo wa kimataifa wa England, huku Gabriel Jesus na Bernardo Silva kila mmoja akifunga bao moja kuwezesha kupata ushindi huo Jumamosi.

"Sifa zote ni kwa (Sterling). Sio tu kwa sababu ya mabao matatu, ni muhimu kwa kile tulichonacho," alisema kocha huyo wa Manchester City akiwaambia waandishi wa habari.

"Maendeleo yake kama mchezaji ni kwa sababu anataka kuimarika zaidi na pia tumefurahishwa na kiwango chake. "Raheem mwenyewe anajua vizuri nini anachotakiwa kukifanya. Ana ushindani mkubwa na mwenye kasi ya kufunga mabao.

"Tuna mawinga wenye akili ya kufunga mabao na hilo ndilo jambo la muhimu zaidi kwa timu."

Ushindi huo wa City kimahesabu umewawezesha kumaliza katika nne bora ya ligi Kuu England, huku zikiwa zimesalia mechi tatu ligi hiyo kumalizika.




# Griezmann kutua England

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Antoine Griezmann anatafuta namna ya kutimka kwenda kutafuta mahali ambapo atapata nafasi ya kucheza na kujiamini ili kurudisha makali yake.

Mfaransa huyo anadaiwa kuwa na mpango wa kwenda ama Manchester United au Manchester City, akiamini huko atapata nafasi ya kurudi kwenye kiwango chake bora.

Mshambuliaji huyo alitua Barcelona akitokea Atletico Madrid kwa ada ya pauni milioni 108 wakati wa dirisha la uhamisho la majira ya joto mwaka jana, lakini amekuwa akihusishwa na mpango wa kuachana na miamba hiyo ya Nou Camp baada ya kushindwa kucheza soka la kiwango kilichotarajiwa.

Kwa mujibu wa Mundo Deportivo, klabu mbili za jijini Manchester nchini England, mara kadhaa zimekuwa zikifuatilia uwezekano wa kunasa huduma ya Griezmann na kwamba anaweza kushawishika kwenda kukipiga kwenye Ligi Kuu England katika dirisha hili la uhamisho wa majira ya kiangazi.

Griezmann amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho nne katika mechi 45 za michuano yote aliyocheza msimu huu, lakini ameanzishwa mechi moja tu kati ya nne za mwisho alizotumikia wababe hao.

Alicheza dakika mbili tu katika sare ya 2-2 dhidi ya klabu yake ya zamani ya Atletico, Jumanne iliyopita.

# Simeone ataka Atletico waimarike zaidi

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone anaangalia uwezekano wa kuimarika zaidi kwa Atletico Madrid licha ya kupata tiketi ya kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara nyingine.

Bao la dakika ya 74 kutoka kwa Diego Costa lilishuhudia Atletico iliyomaliza na wachezaji 10, kuifunga Real Betis bao 1-0 Jumamosi na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa nane mfululizo.

Lakini Kocha Mkuu, Simeone amekataa kumpumzika, na kuitaka Atletico kuendelea kukua zaidi.

"Siwezi kuachambua kile kilichofanywa, na ni lazima wachezaji waimarike zaidi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Mara zote tunataka kuimarika na njia pekee ni kuifanya klabu kuwa na uwezekano wa kucheza vizuri uwanjani na kuendelea kukua kama ilivyokuwa katika miaka ya hivi karibuni.

"Kama kulikuwa na wakati wa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya ni sawa, ilikuwa vile ilivyotokea kwenye mchezo kwa sababu ya sisi.

"Walionekana kutaka kurudi kiwango, lakini wachezaji walicheza kwa kujituma na mwisho wa siku tukapata ushindi."



HABARI MICHEZO

# Messi anatakiwa kumpumzika – Setien

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Quique Setien amesema Lionel Messi anahitaji "kupumzika" huku Barcelona ikizidisha presha kwa Real Madrid baada ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Real Valladolid.

Messi alimtengenezea pande Arturo Vidal aliyefunga bao dakika ya 15 Jumamosi wakati Barca wakipunguza tofauti ya pointi na kuwa moja dhidi ya vinara wa LaLiga, Madrid, ambao wana mchezo mmoja mkononi.

Lakini nyota huyo alicheza kwa dakika zote 90 wakati Barca wakiwa na ratiba ngumu na Setien alisema baada ya mchezo huo kuwa Messi anahitaji kupumzika.

"Pengine atapumzika, ndio," alicheza kocha huyo wa Barcelona akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilimwambia hivyo awali na pengine leo tungepata mabao mengi, lakini tulistahili ushindi, pengine alitakiwa kupumzika."

Antoine Griezmann na Luis Suarez, kila mmoja alicheza kwa dakika 45, huku raia huyo wa Uruguay akichukua nafasi ya raia huyo wa Ufaransa katika kipindi cha pili.

Setien, ambaye alisema Griezmann "ameshuka kiwango", anahisi Barca walikuwa wamechoka baada ya mchezo wa tatu ndani ya wiki moja.

"Nafikiri miguu ya wachezaji ilichoka. Si zaidi ya dakika 72 tangu tulipocheza mchezo wetu wa mwisho," alisema.







# SANCHO NJIA NYEUPE UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeandaa ofa ya pauni milioni 50 ili kuhakikisha wanaipata saini ya winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho.

Winga huyo anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 100 kwenye mkataba wake wa sasa unaotarajiwa kufikia tamati mwaka 2022.

Suala hilo limeifanya Dortmund kuanza kutafuta mbadala wa mchezaji huyo kwa kuwa wanaamini United inaweza kufanikiwa kutoa kiasi cha fedha wanachohitaji.

Inaelezwa kuwa Dortmund huenda ikawa tayari kupokea pauni milioni 50 ikihofia kumpoteza bure wakati msimu ujao utakapofikia tamati.

United imekuwa ikiifuatilia saini ya mchezaji huyo kwa muda mrefu ambapo wamekuwa wakipambana na Real Madrid wanaotajwa kuwa kwenye mpango wa kuhakikisha wanaipata saini ya fundi huyo.

Sancho mwenye umri wa miaka 20, amekwishaweka wazi anatamani kujiunga na United dirisha lijalo ikiwa makubaliano kati ya pande hizo yatafikiwa.

# Jorginho kupishana na Ramsey Chelsea

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri bado anataka kuisuka upya Juventus kupitia kwa kiungo Jorginho na anataka kumtumia kiungo wake, Aaron Ramsey kama chambo.

Sarri ndiye alimnunua Jorginho wakati akiinoa Chelsea na sasa anataka kuungana naye kwenye kikosi chake cha Juventus.

Kwa sasa Jorginho ameonekana kuwa mchezaji wa kawaida kwenye kikosi cha Kocha Frank Lampard na Sarri anataka kumrejesha Italia ili kuunga naye.

Ramsey aliyejiunga na Juventus msimu uliopita baada ya kuachana na Arsenal, anaweza kurejea katika Ligi Kuu England kama mpango huo utafanikiwa lakini, safari hii akivaa jezi ya Chelsea.

Ripoti kutoka Italia zinasema kuwa, Chelsea wanaweza kufanya biashara ya wachezaji hao na Sarri wakati huu ambao, Lampard yuko 'bize' kukisuka upya kikosi chake akinasa mastaa wawili wakali, Timo Werner na Hakim Ziyach.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KOULIBALY AAMUA KUSTAAFIA NAPOLI

## ●●● Licha ya klabu kubwa Ulaya kuwania saini yake ikiwamo Barca, United, City, PSG...

**NAPLES,** Italia

BEKI wa kati wa Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly, amemaliza tetesi zinazoendelea kuhusiana na mpango wa kutaka kuondoka Napoli wakati wa majira ya joto kwa kusema atastaafia soka akiwa na klabu hiyo.

**Kwa muda mrefu beki huyo ghali anahusishwa na mipango ya kutaka kuondoka klabuni hapo, huku Manchester City na Manchester United zote zikitajwa kuhitaji huduma ya beki huyo wa kati ambaye yuko katika kiwango cha juu.**

Mabingwa wa Ligi Kuu England Liverpool, Barcelona na Paris Saint-Germain pia nazo zimetajwa kuonyesha nia ya kumsajili mlinzi huyo.

Lakini gazeti liitwalo Gazetto dello Sport limeandika mchezaji huyo ameweka wazi uamuzi wake wa kuona anastaafia katika klabu hiyo kongwe nchini Italia.

Koulibaly aliliambia gazeti hilo la Italia: "Sijawahi kuzungumza na Napoli kuhusiana na kutaka kuondoka. Kama tutatakiwa kutafuta suluhisho tutafanya hivyo, lakini sijawahi kuzungumzia kuhusiana na dirisha la usajili.

"Mimi pia ninasoma kwenye magazeti kuhusiana na hatima yangu. Lakini kwa sasa mimi ninataka kufikiria kuhusu kucheza tu, nina asilimia 100 ya kuitumikia Napoli na inanikera kusikia ninahusishwa na uhamisho, kila siku unasikia hili au klabu nyingine ya Ulaya.

"Tutaangalia nini Rais (Aurelio De Laurentiis) ataamua kuhusiana na hili au kama atafikia uamuzi wa kuongeza mkataba wangu, hii itanifanya mimi kustaafia kandanda hapa."

Koulibaly amekuwa hajakosa mechi hata moja ya Napoli tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2014 akitokea Genk na sasa amekuwa mmoja wa mabeki wa kati bora duniani. Katika kipindi cha miaka sita, beki huyo ameichezea klabu hiyo mechi 239 na amekuwa mchezaji mwadilifu kwa wakati huu licha ya kutakiwa na klabu kubwa za Ulaya.

Huku Manchester City na Manchester United zikijiandaa kuimarisha safu zake za ulinzi, inaeleweka kwa nini zimevutiwa na beki huyo mwenye umri wa miaka 29.

Hata hivyo, zitatakiwa kujiandaa kupambana ili kumwondoa beki huyo mjini Naples.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUIKAMUA UNITED

BORUSSIA Dortmund haitapokea ada chini ya pauni milioni 116 ili kumruhusu winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), ambaye anatajwa kuwindwa na Manchester United. ***(Westdeutsche Allgemeine Zeitung, via Manchester Evening News)***

### BARCA YAKATA TAMAA

BARCELONA imekata tamaa kuhusiana na kukamilisha mchakato wa kumrejesha mshambuliaji wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar (28), kwenye Uwanja wa Nou Camp majira ya joto mwaka huu. ***(Marca)***

### JOVIC ANUKIA LEICESTER

LEICESTER City inataka kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Serbia, Luka Jovic (22), kutoka Real Madrid kwa ada ya pauni milioni 31 ili kucheza pamoja na Jamie Vardy katika msimu ujao. ***(Mail on Sunday)***

### GERRARD ATAKIWA BRISTOL

KLABU inayoshiriki Ligi ya Championship, Bristol City inataka kumwajiri Kocha wa Rangers, Steven Gerrard ili kuchukua mikoba iliyoachwa na Lee Johnson, ambaye ametimuliwa. ***(Sunday Express)***

### THIAGO AGOMBEWA ULAYA

JUVENTUS na Manchester City zimeungana na Liverpool katika mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Hispania, Thiago Alcantara, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Tuttomercatoweb - in Italian)***

### CHELSEA, INTER VITANI

CHELSEA na Inter Milan zimeanza mazungumzo na Lille kuhusiana na uhamisho wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Jonathan Ikone, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Le 10 Sport - in French)***

### ZIDANE AMHOFIA RODRIGUEZ

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema hana uhakika kama kiungo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), ataichezea tena klabu hiyo. ***(AS)***

### ZANIOLO AGOMBEWA ITALIA

JUVENTUS na Inter Milan zimeonyesha nia ya kumsajili kiungo mshambuliaji wa Roma na Timu ya Taifa ya Italia, Nicolo Zaniolo, ambaye ana umri wa miaka 21, katika majira ya joto mwaka huu. ***(Tuttosport - in Italian)***

### BARCA KUILIPA DORTMUND

BARCELONA italazimika kuilipa klabu ya zamani ya Ousmane Dembele, ambayo ni Borussia Dortmund kiasi cha pauni milioni 17.9 kama itamuuza mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa ambaye ana umri wa miaka 23, katika majira ya joto. ***(Bild - in German)***

### PELLEGRINI AMTAKA DIAZ

KOCHA mpya wa Real Betis, Manuel Pellegrini amesema anataka kumsajili kwa mkopo kiungo wa Real Madrid, Brahim Diaz (20) kwa ajili ya msimu ujao. Pellegrini aliwahi kufanya kazi na Diaz alipokuwa katika klabu ya Malaga. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

## Sare mfululizo zaitesa Kipanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Kipanga, Rashid Lato, amesema sare ya nne mfululizo katika Ligi Kuu Zanzibar inamweka katika wakati mgumu wa kutimiza malengo yake wakati ligi hiyo ikielekea ukingoni.

Kipanga ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lato, alisema wachezaji bado hawajapata nguvu na kasi ya kubabiliana na ushindani kwenye ligi hiyo tangu iliporejea tena kutoka katika mapumziko mrefu yaliyosabibshwa na virusi vya ugonjwa corona.

Lato alisema baadhi ya wachezaji wanaonekana walizembea kufanya mazoezi binafsi na sasa hali hiyo inawafanya washindwe kuonyesha kiwango bora.

"Bado kikosi hakijachanganya vizuri, mechi zinavyoendelea, tunaona wachezaji wanajituma lakini bado wamekuwa wagumu wa kufanya uamuzi pale wanapopata nafasi, hii yote inasababishwa na kutofanya mazoezi wakati ligi ilipisimama, ni wazi wakati wa mapumziko wao walibweteka," alisema Lato.

Kocha huyo alisema muda wa wiki mbili wa kufanya mazoezi ya pamoja uliotolewa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), haukutosha kuwaimarisha wachezaji wake.

## Sahare yatolewa, yashuka daraja

**Na Adam Fungamwango**


KLABU ya Sahare All Stars iliyokuwa inashiriki Ligi Daraja la Pili imesema imekubaliana na matokeo ya kufungwa katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, dhidi ya Namungo FC, kushuka daraja.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kessy Abdallah, alisema katika mechi ya nusu fainali kati yao dhidi ya Namungo walicheza vizuri, lakini kosa moja walilofanya ndilo ambalo liliwaadhibu.

"Tunawapongeza wenzetu, tunawatakia kila la kheri, mechi ilikuwa nzuri, kila timu ilicheza vizuri, lakini wenzetu walitumia kosa moja tulilofanya na kutuadhibu, ndiyo mpira," alisema kocha huyo.

Sahare All Stars ilichapwa bao 1-0 na Namungo katika mchezo wa hatua ya nusu fainali uliochezwa juzi Jumamosi kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga na kuyaaga mashindano hayo yanayotoa tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF).

"Wala hatutii huruma, kufungwa mechi ya nusu fainali na kushuka daraja siyo kigezo cha sisi kukata tamaa. Kuna timu zimecheza Daraja la Kwanza kwa miaka 15 zipo hapa hapa hazipandi na wala hazishuki, sisi tumeshuka na nina uhakika msimu ujao tutapanda daraja, na tutaziacha na kwenda kucheza Ligi Kuu," alitamba kocha huyo.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba (kushoto), akimkabidhi mshindi wa Multibet, George Siwale mfano wa hundi ya Sh. milioni 9.9 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 18 huku akitumia kiasi cha Sh. 8,500 kuweka ubashiri wake. **NA MPIGAPICHA WETU**

# AZAM YAPANIA KUJIFUTA MACHOZI LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Aristica Cioaba, amesema wamedhamiria kuhakikisha wanamaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ili kuweka heshima.

**Kauli hiyo ya Cioaba imekuja baada ya timu yake kuvuliwa ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA, na hivyo kupoteza tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Cioaba alisema anaendelea kuimarisha mikakati ili kikosi chake kifanye vema katika mechi zilizobakia licha ya kuwakosa baadhi ya wachezaji wake nyota wa kikosi cha kwanza.

Cioaba alisema baada ya kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA, nguvu zao zimeelekea katika kulinda heshima yao katika ligi hiyo ambayo mwakani itashirikisha timu 16 tu.

"Tumepoteza nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa, hali hiyo haitaturudisha nyuma kupambana kutafuta alama tatu katika mechi zetu zote zilizobaki, wachezaji wanalifahamu hilo, tutapambana timu kutafuta matokeo mazuri," alisema Cioaba.

Aliongeza anafahamu hakuna mechi rahisi kwa sababu kila timu inahitaji kutimiza malengo yake, huku vita kubwa ikiwa kwenye klabu zinazopambana kujinasua na janga la kushuka daraja.

"Wachezaji wanatakiwa kujituma kwa sababu hatujafikia malengo yetu, vijana wangu walicheza vizuri dhidi ya Mwadui FC, matokeo yake yametuimarisha na tunataka kuendeleza kasi ile," aliongeza kocha huyo.

Azam ina pointi 65 na iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo nyumba ya mabingwa Simba yenye pointi 81, huku Yanga ikishinda nafasi ya tatu, huku kila timu ikibakiwa na mechi nne ili kumaliza msimu 2019/20.

# *Namungo yaanza mikakati ya fainali*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, amesema atalazimika kufanya mabadiliko katika safu yake ya ushambuliaji kutokana na nyota wake tegemeo kuwa majeruhi.

Mipango hiyo ya Hitimana ni kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City itakayochezwa keshokutwa pamoja fainali ya Kombe la Shirikisho FA itakayofanyika Agosti 2, mwaka huu.

Juzi Namungo ilifanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sahare All Stars inayoshiriki Ligi Daraja la Pili ya jijini, Tanga.

Bao pekee la Namungo katika mchezo huo lilifungwa na Edward Manyama dakika ya 80 na sasa watasubiri mshindi kati ya Simba na Yanga ambao walitarajia kukutana jana jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema amefurahi kuona timu yake imetinga fainali ya michuano hiyo, hivyo atalazimika kufanya mabadiliko katika kikosi chake ushambuliaji ili kuhakikisha wanashinda mechi zilizobaki za Ligi Kuu pamoja na kuchukua kombe la FA.

Hitimana aliwataja wachezaji wake ambao ni majeruhi kuwa ni pamoja na washambuliaji, Blaise Bigirimana, Reliants Lusajo, Hashim Manyanya na kiungo, Steve Nzingamasabo.

"Kwangu yoyote nitakayekutana naye sawa, ila kama Simba atapita fainali itakuwa balaa, ninatakiwa kuwa makini, kwa sababu wana timu nzuri na bora kwa soka la Tanzania, lakini itatupa urahisi kwetu kujipanga kucheza kimataifa," alisema Hitimana.


Kocha huyo aliongeza bado pia anataka kuona kikosi chake kinamaliza kwenye nafasi ya pili katika Ligi Kuu Bara msimu huu.

Michezo
Jumatatu Julai 13, 2020
Nipashe



Koulibaly aamua kustaafia Napoli

UKURASA 22



Kiungo wa Simba, Clatous Chama (katikati), akijipanga kuwatoka nyota wa Yanga, Said Makapu (kushoto) na Papy Tshishimbi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 4-1. **PICHA : JUMANNE JUMA**

## Tanzania chali, Uganda yapeta

**Na Saada Akida**

RUFANI ya Tanzania dhidi ya majirani zao Uganda kutumia wachezaji wenye umri mkubwa katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa wasichana wa umri chini ya miaka 17 imefeli, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema rufani yao iliyokuwa inalalamika Uganda kutumia wachezaji watano wenye umri mkubwa 'imegonga mwamba' na hivyo Uganda itasonga mbele katika mashindano hayo.

Kidao alisema wamepokea kwa huzuni majibu ya rufani hiyo kwa sababu wanaamini Uganda ilitumia wachezaji 'vijeba'.

"Ni kweli majibu yametoka na tumeshindwa, hivyo Uganda wameshinda, nadhani hivi karibuni tutaliweka wazi hili," alisema Kidao.

Kiongozi huyo amewataka wadau wa soka la wanawake kuendelea kuziamini timu zao zote na shirikisho litaendelea kujipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano ambayo bado hawajatolewa.

Yosso wa Tanzania waliondolewa katika mashindano hayo baada ya kuchapwa mabao 5-0 katika mchezo wa marudiano ugenini Kampala wakati nyumbani walipata ushindi wa magoli 2-1.

# SIMBA BABA LAO

### Yaichapa Yanga mabao 4-1 na kuzima ndoto zao za kushiriki michuano ya CAF, Namungo haooo...

**Na Saada Akida**

WAMELIPA Kisasi! Simba imeendelea kung'aa baada ya kufanikiwa kuifunga Yanga mabao 4-1 katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa jana jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

**Mbali na kutoa kichapo, Simba imeinyima Yanga tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao, na hivyo sasa mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara watakutana na Namungo katika fainali itakayochezwa Agosti 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa.**

Mbrazil Gerson Fraga ndiye aliifungia Simba bao la kwanza katika mchezo huo baada ya kumalizia kazi nzuri iliyofanywa na Clatous Chama ambaye kabla ya kutoa pasi, aliwazungusha wachezaji wawili wa Yanga, Said Makapu na Papy Tshishimbi.

Bao hilo lilidumu mpaka timu hizo zilipokwenda mapumziko katika mchezo huo uliokuwa na kasi pamoja na ubabe kutoka kwa wachezaji wa timu zote mbili.

Chama ambaye alikuwa katika kiwango chake jana, alifunga bao la pili baada ya kuanzisha shambulizi na kumpatia Bocco, halafu nahodha huyo akamrejeshea mfungaji huyo dakika ya 48 ya mchezo huo.

Simba ikiendeleza ubora wake ilipata bao la tatu kupitia kwa Luis Miquesson ambaye aliwahi mpira wa kichwa uliookolewa na Tshishimbi ambaye alikuwa anaondoa hatari kwenye lango la timu yake dakika ya 51.

Kiungo Muzamiru Yassin aliyeingia akichukua nafasi ya Fraga alimalizia mpira uliotemwa na Menatha ambaye alishindwa kudaka shuti la Meddie Kagere na hivyo kuiandikia Simba bao la nne ambalo liliwanyamazisha mashabiki wa Yanga waliokuwa wanaamini wanaweza kupindua matokeo.

Yanga ndio ilikuwa ya kwanza kufanya shambulizi katika lango la Simba kupitia kwa David Molinga, lakini beki wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kennedy Juma aliwahi kuruka na kuokoa shambulizi hilo kwa kichwa na mpira kwenda nje dakika ya nne.

Simba walijibu shambulizi hilo dakika mbili baadaye kwa kufanya kashikashi katika lango la wapinzani wao, lakini golikipa wa Yanga, Menata Mnacha alikuwa makini kwa kupangua shuti kali lililopigwa na kiungo, Jonas Mkude.

Dakika ya sita, winga hatari wa Simba alipoteza nafasi ya kufunga baada ya kupiga juu ya lango na kupoteza pasi aliyopewa na Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr'.

Nahodha wa Simba, John Bocco alimpa pasi fupi Chama lakini Mzambia huyo aliinyima Simba nafasi ya kupata bao la mapema baada ya shuti alilopiga kupaa juu, huku tayari mabeki wa Yanga wamemwacha huru kufanya shambulizi hilo ndani ya eneo la hatari huku Bocco naye akikosa goli kwa kupiga pembeni dakika ya 31.

Aishi Manula 'Tanzania One' aliinyima Yanga nafasi ya kusawazisha baada ya krosi nzuri aliyopiga iliyokuwa inaelekea langoni kuishia mikononi mwa Tanzania One huyo dakika ya 34 huku Lamine Moro akiokoa hatari nyingine langoni mwao kupitia mpira uliopigwa na Miquissone.

**YANGA YATANGULIA**

Saa 9: 02 mchana; Kikosi cha Yanga kilikuwa cha kwanza kuingia uwanjani kwa kutumia gari mbili aina ya Coaster huku basi lao kubwa lililozoeleka likiingia tupu.

Dereva wa Yanga aliingia na basi hilo akiwa peke yake na kwenda kuliweka kwenye sehemu maalumu ya maegesho.

9:18 mchana; Kikosi cha Simba kilitinga kwenye uwanja huo wa kisasa nchini kikiwa kwenye busi lao na wachezaji wake wote pamoja na benchi la ufundi.

Licha ya serikali kutangaza kuuza tiketi chache ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, mashabiki wa Simba waliendelea kuwa wengi zaidi uwanjani hapo wakiwa wamevalia jezi za rangi nyekundu na nyeupe.

9 770856 541002 >